

KUNG'ANG'ANIA



Shukrani. Asante, Ndugu Joseph. “Sasa naamini.”

Sasa naamini, sasa naamini,
Mambo yote yawezekana, sasa naamini;
Sasa naamini, sasa naamini,
Mambo yote yawezekana, sasa naamini.

² Hebu tuinamishe mioyo yetu sasa katika Uwepo Wake. Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe tena, usiku wa leo, kwa sababu kwamba Wewe umekuwa pamoja nasi kote katika siku, na umeongoza hatua zetu. Na sisi tumekusanyika pamoja tena, usiku wa leo, katika Jina la mpendwa Bwana Yesu. Na sisi tupo hapa chini ya matarajio makubwa. Tunatazamia sasa ule wakati ambapo Wewe utatupatia kilele cha mkutano huu, kwamba wakati Wewe utakapoponya wagonjwa, watu wote wanaoteseka usiku wa leo. Jalia kusiwe na mtu mnyonge atakayesalia miongoni mwetu usiku wa leo. Jalia imani yao ipande juu, Bwana, kutoka...na wasiangelie shida zao tena, ila Yule Ambaye ndiye suluhisho, au tiba, kwa shida zao. Pia, Mungu, tunaomba kwamba Wewe utatumegea Mkate wa Uzima, upya, kutoka kwenye Neno Lako, ambalo litatutia moyo. “Kwa kuwa imani huja kwa kusikia, na hilo Neno la Mungu.” Na sisi tutakusifu Wewe, kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

³ Ketini. Nina furaha sana kuwa hapa tena usiku wa leo. Ndiyo kwanza nipitie mlangoni pale nje, dakika chache zilizopita, na kulikuwa na umati mkubwa wa watu wakizunguka bila mpango, wakitembea huku na huko mitaani. Na de—dereva wa basi akasema kwamba, ama nanii... Samahani. Dereva wa teksi akasema, “Watu hao hawakuja kanisani, sivyo?” Nikasema, “Naam, bwana. Hawawezi kuingia,” Nikasema. Watu wamedai kwamba watu hawapendi kwenda kanisani. Unaona? Bali wao—wao... Ninaamini kwamba Injili ingali ndiyo—ndiyo nguvu kuu kuliko zote za kuvuta zilizoko duniani, hata hivyo katika urahisi Wake.

⁴ Tulikuwa na wakati mzuri sana kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara wa Full Gospel asubuhi ya leo. Bwana alitubariki. Alikutana nasi huko kwa njia kuu. Walikuwa wameuza, naamini walisema, tikiti elfu moja mia saba, na wakaruhusu mia tatu zaidi kuingia ndani, ndipo basi wasingeweza kuruhusu mwingine zaidi kuingia ndani, nao wakasimama kwenye marefu na karibu na milango. Ndipo—ndipo Bwana, wakati tulipofanya wito wa madhabahuni, alitupatia wengi, kusimama, kupokea Uzima wa Milele. Kwa hiyo tunashukuru sana kwa hilo.

⁵ Na—na halafu ninataka kumshukuru ndugu fulani. Asingeweza kuingia kule nje, sidhani. Na yeye—yeye alimpa Billy, muda mfupi uliopita, ktoni ya risasi za .22, kwa ajili yangu. Na mimi ninazo hapa nyuma. Nitazifurahia, hakika. Asante sana, kama uko nje na unaweza kusikia hilo, ama ndani, popote pale. Mimi hakika. . .

⁶ Hiyo imekuwa ni baraka kubwa kwangu, wakati mwingine, kulenga shabaha. Na, sasa, inakubidi kuwa na kitu fulani ili kwa namna fulani kutoa presha. Na kwa hiyo hivyo ndivyo mimi hufanya, wakati mwingine nikipata nafasi, na ninaweza, mbona, ninakimbia kwenda kwenye uwanja wa shabaha na kulenga shabaha kwa muda kidogo, ili tu kutoa mvuke. Wewe. . . Ninaamini Yesu alisema, “Hebu tujitenge tuingie nyikani kwa kitambo.”

⁷ Sasa, tunakupenda sana! Na kesho ni Jumapili, na kila mtu anataka kwenda kanisani Jumapili. Na mimi ninajua, ama nina hakika kabisa, nyinyi nyote mnajua mahali ambapo—ambapo (ninajaribu kusema kanisa la mwamba, ndivyo) Kanisa la Mwamba lilipo. Hilo ndilo kanisa ambalo linadhamini mkutano huu, nadhani, na mengine yanazuru hapa. Na nyinyi wageni mlio nje ya mji, ambao mmekuja kwenye mkutano, na msiponinii. . . Sasa ikiwa una mahali pa wajibu, wewe nenda hapo. Hilo ndilo unalopaswa kufanya. Daima simama mahali pako pa wajibu. Huo ni—huo ni wajibu wako kwa Mungu na kwa mchungaji wako, kwa kusanyiko lote. Lakini ikiwa huna mahali popote pa kwenda, nina hakika utakaribishwa hakika kwenye Kanisa la Mwamba, kwa ajili ya. . . Nadhani wamezitangaza ibada.

⁸ Na—na nyinyi watu mnaookoka katika mikutano hii, hatujui kamwe. Sasa, kwa kawaida sisi hufanya wito wa madhabahuni, kile tunachokiita wito wa madhabahuni, unaona, na hilo ni—hilo ni sawa. Sina chochote dhidi ya hilo. Hilo ni jema. Bali ninaamini, kama utakumbuka Maandiko, wao—wao hawakuwa na wito wa madhabahuni. “Wote walioamini, unaona, waliongezwa kanisani.” Waaminio!

⁹ Basi—basi ikiwa huna kanisa, vema, nina hakika kwamba Ndugu Vick angekukaribisha katika kanisa lake, au yeyote wa hawa wanaume karibu hapa. Kama hujapata ubatizo wa Kikristo bado, shauriana nao. Na usikome. Dumu tu kuendelea, endelea tu kukaza mwendo.

¹⁰ Kamwe hatujui, hata hatujui ni wangapi wameponywa. Na nyinyi wachungaji, ndugu, kumbukeni tu, wakati mkutano ukimalizika, labda majuma, mtu fulani anakujia, kama maskini mama, na aseme, “Unajua, nilikuwa na shida ya kina mama. Haipo tena.” Mtu fulani, “Mimi—mimi, unajua, mara ghafla, sikutaka sigara tena. Zote ziliniacha tu.” Unaona? Wao, wanaponywa, wengi sana, huwezi kuwaita. Unaona, ni kila mahali tu. Na sijakuwa na mkutano bado ila ambao hayo

yalikuwa ndiyo matokeo baadaye, ambapo Bwana aliponya watu na hawakujua hilo papo hapo, bali wao—walipata afya. Na muda si muda wajua, walikuwa, wanasimama tu na kuondoka, na yote imekwisha. Lakini labda hawaelewi hilo papo hapo, bali, ni, pole pole inaisha.

¹¹ Ninakumbuka, huko Ufini, muda mrefu uliopita. Nadhani kuna Wafini hapa. Kulikuwa na mvulana mdogo alikuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu. Labda mlisoma—mlisoma kitabu chake. Habari zilienea, kote katika Urusi. Bali niliona hilo katika ono kabla halijatukia, miaka miwili, na kulitangaza kote katika taifa.

¹² Ninamkumbuka maskini msichana yule wa Kifini, usiku ule akisimama huko nje katika ukumbi, na yeye alikuwa na mguu mmoja yapata inchi sita au nane mfupi kuliko huo mwingine. Alikuwa na kiatu kikubwa kilichoshonwa, huku a—amejifungia ukanda, na mmoja kwenye kidole chake cha mguu, kulabu ndogo. Na alikuwa na m—mshipi juu ya bega lake, na ukaja huku namna *hii* na kuteremka hadi kwenye kidole cha kiatu chake. Alikuwa na magongo mawili. Na maskini jamaa mdogo aliyeonekana mchafu. Na kila wakati angejaribu kusonga, ingembidi kuinua mguu huo kwa bega lake, ule ukanda; na halafu ausukume namna *hiyo*, na kuuweka chini, halafu basi aweke chini gongo. Na ilitubidi ku . . .

¹³ Tulikuwa kwenye kile wanachokiita (sasa ndugu wa Kifini, dada hapa, si—sitamki hili vizuri) Messuhalli, nalo lilichukua alfabeti zote. Na wao wangeruhusu yapata elfu ishirini kuingia ndani, ama chochote kile kilichokuwa; na halafu waliwaruhusu kutoka nje, na kisha wanifanye kuzungumzia elfu ishirini wengine.

¹⁴ Na mvulana mdogo alikuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu, huko Kuopio, aliyekuwa ameuawa na motokaa. Na, loo, jamani! Hawatangazi muziki wa roki na kadhalika huko, ni habari tu na kadhalika, kwa hiyo hili liliingia kwenye habari. Ndipo wakaja kote kutoka Urusi, wakaingia huko juu.

¹⁵ Ndipo, niliona, usiku huo. Hiyo ilikuwa ni punde tu baada ya vita, yapata miaka mitano, nadhani, baada ya vita. Ndipo niliona askari wa vita wa Urusi na askari wa vita wa Ufini, huku wamekumbatiana, wakipendana, wakipigana kikofi cha kuonyesha upendo mmoja na mwenzake. Chochote kitakachomfanya Mrusi kumpiga Mfini kikofi cha kuonyesha upendo, kitatuliza vita, hicho kinahitaji upendo wa Yesu Kristo kufanya hivyo.

¹⁶ Lakini wale askari wakubwa mashuhuri wa kikomunisti wamesimama pale! Tulipita karibu na kundi la maskini askari wa vita wa Ufini, maskini jamaa hao hawakuwa wamenyoa bado, nyuso tu zinazong'ara, huku wamevaa hizo buti kubwa kubwa, wakiteremka mtaani, wakiangalia watu. Walikuwa tu

wamejaa pande zote, kwa majengo ya mji. Na hao askari wa vita wakiwa wamesimama miguu sawa, machozi yalitirika mashavuni mwao. Wakasema, “Tutampokea Mungu anayeweza kuwafufua wafu.” Unaona? Wao ni wanadamu kama tulivyo sisi.

¹⁷ Lakini jambo ni kwamba, chochote kinachokiri Ukristo na hakileti matokeo yoyote, wanakiweka kando. Wanataka uhalisia fulani. Unaona, hiyo ndiyo sababu ukomunisti umeinuka, kwa sababu ya kupungukiwa kwa kanisa. Kanisa lina hatia ya ukomunisti, kwa sababu lilikuwa ndilo lililoachilia. Na sasa hebu wazia, asilimia moja tu ya Urusi sasa ni ukomunisti, asilimia moja. Asilimia tisini na tisa ya watu wangali ni Wakristo. Kile wanachohitaji ni kuwaka Moto kwelikweli, pamoja na nabii akiwa na BWANA ASEMA HIVI. Hilo, unaona, hilo lingesukuma nguvu za ukomunisti kuingia baharini. Tunachohitaji, ni, wanahitaji Ukristo halisi.

¹⁸ Na hawa askari wa Kirusi wakisimama pale usiku ule, nikaingia kwenye baraza ndogo na kuingia kwenye maskini ukumbi. Na msichana huyu mdogo, kamwe sitamsahau, alikuwa—alikuwa na maskini nywele zisizochanwa na sketi zilizopasuka. Na yeye alikuwa ametoka kwenye choo—choo cha wanawake. Na wao waliambiwa wasinisumbue.

¹⁹ Ningetoka nje mtaani na kununua peremende. Ni—ninao watoto, mwenyewe, na ni—ninapenda watoto. Nafikiri mtu yeyote asiyependa watoto, wana kasoro fulani. Na kwa hiyo maskini jamaa hawa, ningekuwa na msururu urefu wa nusu jengo, ukunifuata. Ningewapa peremende. Wangenipatia kiasi fulani cha zile fedha pale, na hazikufaa kitu hapa, bili kubwa mno namna hiyo, nami ningenunua peremende. Sijui nilichokuwa ninanunua, bali niliwapa hicho. Ndipo basi wakawauliza mitaani, mnajua, kama nilitembea karibu, ili tu kuendelea na kunipuuza, nadhani, ili kupata zoezi kidogo.

²⁰ Na ndipo wakati nilipoingia usiku huo, maskini msichana huyo alidhanja alikuwa amefanya kosa fulani, na ninajua alikuwa ameinamisha maskini kichwa chake. Ndipo akaangalia juu kutoka kwa maskini macho yake ya samawati, na alikuwa anaenda kuona kile nilichokuwa ninaenda kusema.

²¹ Nao askari wawili mbele yangu, walikuwa wamefika mlangoni. Na wao walikuwa wanaimba *Amini Tu*. Wawili zaidi walikuwa nyuma yangu. Nikawaashiria, “simama.”

²² Nilitaka kuona kile ambacho mtoto huyo angefanya. Alikuwa yapata, nakisia, yapata umri wa miaka minane, kumi. Nilifahamu baadaye, alikuwa maskini, yatima wa vita, wa Kifini. Baba yake na mama walikuwa wameuawa katika vita vya Urusi. Na kwa hiyo ni—nilimtazama maskini jamaa huyo, na—naye alikuwa na haya magongo. Na yeye akafikiria kuwa ningeninii. . . alikuwa amefanya jambo baya, mnajua.

²³ Ndipo nikamtazama. Nikasema, “Unataka kuniona?” Na, bila shaka, asingeweza kuelewa Kiingereza. Ndipo nikamwashiria kidole changu, kuja pale. Ndipo akainua kichwa chake na kutazama kidogo kwa njia ya kitoto. Akatoa maskini haya magongo, na kuinua maskini mguu wake, kwa namna fulani namna hiyo. Na hapa akaja, akitembea.

²⁴ Nikawaza, “Nitaona tu kile anachofanya mtoto huyo.” Nami nikasimama tu hapo namna *hiyo*. Na yeye akanikaribia kabisa, na akanitazama; na kutazama juu namna *hiyo*, na kutazama chini. Nikawaza, “Nitaona tu kile anachofanya.” Ndipo akachukua koti langu, akalitazama mkononi mwake, na kubusu mfuko wa koti langu, na kuweka chini mkono wake.

²⁵ Niliikuwa ninaenda kumwambia, “maskini dada yangu,” sikujua jinsi ya kuongea. Ndipo nikaangalia mbele, nikamwona akikimbia kuteremka mtaani, kawaida tu kama mtoto yeyote. Ndipo nikasema sasa, nisingeweza kuongea na yeye, nikasema, “Mpenzi, Yesu Kristo anakufanya mzima.”

²⁶ Na yeye akavuta maskini sketi yake, maskini Mfini asili, na kusema, “Kiitos.” Hiyo inamaanisha, “asante,” unaona, kwa kubusu mfuko. Ni—ninaamini, kama ningalikuwa ndiye mnafiki mkubwa kuliko wote ulimwenguni, Mungu angeiheshimu imani ya mtoto huyo.

²⁷ Na kwa hiyo yeye, niliwaza, “Vema, yeye ataipata, baada ya kitambo, hata hivyo. Unaona, itaendelea, atakuwa sawa, maana nilikuwa nimemwona katika ono.” Lazima iwe! Ninachosema, hakina budi tu kuwa.

²⁸ Kwa hiyo usiku huo, kulikuwa na mambo mengi sana ambayo Bwana alikuwa amefanya, na nilikuwa karibu kabisa kuondoka. Ndipo nikasema, “Vema, waite tu wengine wachache.”

²⁹ Naye ndugu yangu akasema, “La,” kasema, “una...” Na Ndugu Baxter akasema, “Umechoka sasa, Ndugu Branham.” Kasema, “Sasa, wewe ninii—wewe ondoka tu sasa, endelea, maana inatubidi kuenda mahali pengine.” Tena kasema, “Wewe ninii tu...”

³⁰ Nikasema, “Vema, ninajisikia tu labda kuwa na yapata wanne au watano zaidi, kuna wengi sana hapa.”

³¹ Na kwa hiyo aliyefuata katika mstari wa maombi alikuwa ni huyo msichana mdogo. Bwana anajua tu jinsi ya kufanya mambo sawasawa kabisa. Kwa hiyo nikasema, “Bibi Isaacson...” Huenda yupo hapa sasa. Alikuwa ndiye sauti yangu ya Ufini. Na kwa hiyo nikasema, “Sasa wewe sema tu maneno ninayosema.” Akasema, “Vema.”

³² Na mimi nikasema, “Mpenzi, Bwana Yesu alikuponya, akakupa tuzo huko nje, kwa ajili ya kile ulichofanya.” Nikasema, “Sasa wewe nenda huko na baadhi ya hao wanaume waivue

hiyo mikanda ya kuning'iniza. Angalia tu kinachotendeka." Ndipo akachechemea kupitia jukwaani. Na mimi nikaendelea na wengine.

³³ Katika dakika chache, hapa akaja na viatu, mikanda ya kuning'iniza juu ya kichwa chake; akiwa mzima kabisa, miguu yote miwili ikiwa sawa iwezekanavyo, huku akikimbia juu-chini kwenye vipandio. Unaona, imani, imani, upendo hupata mahali pake. Hiyo ni kweli.

³⁴ Nilikuwa na tukio dogo leo hii, na kuwaonyesha tu kile ushirika unachomaanisha. Mimi, mara ya mwisho hapa New York, ama nilikuwa hapa kwa Ndugu Hudson, nafikiri, katika. . . Hiyo, sidhani hiyo ilikuwa katika New York. Hiyo ni, sijui ni ipi New York hapa karibu. Na New York wote tu, kwangu mimi, kote kuanzia Tucson hapa, inaonekana.

³⁵ Kwa hiyo basi nilikuwa nikija hapa na Dada Brown na Ndugu Berg. Nina hakika wengi wenu mnawafahamu. Na mimi nimekuwa nikijaribu kumpata maskini huyo mtakatifu, kwa siku moja au mbili zilizopita. Na hakukuwa na mtu kanisani, na ndipo leo hii nikampata kwenye simu. Nilimpata bawabu. Na, vema, nilifikiria nilikuwa nikiongea na msichana mwenye umri wa miaka kumi na sita, ana ujana mwingi sana katika sauti yake. Nikasema, "Dada Brown, usingeweza kukisia, katika—katika mwezi mmoja wa Jumapili, kuwa huyu ni nani."

Ndipo akasema, "Ubarikiwe moyo wako, hakika nisingeweza."

³⁶ Huku akiwa na furaha tu kadiri alivyoweza kuwa. Nikasema, "Ndugu Branham," ndipo akaanza tu kupiga mayowe; maskini kitu cha kupendeza namna hiyo.

³⁷ Na yeye ana umri wa miaka themanini na tatu, na anahubiri mara mbili kwa wiki. Na ninafikiria tu, yeye aliingia hudumani kabla sijazaliwa. Na nilikuwa karibu kusalimu amri; nilifikiria nilikuwa ninazeeka sana, mwajua. Nilipata ujasiri mpya.

³⁸ Ndipo nikamwambia nilikuwa hapa na Ndugu Vick hapa. Na mambo mazuri aliyosema kuhusu Ndugu Vick! Nakuambia, hilo—hilo hufanya. . . Huo ni Ukristo halisi. Yote mawili makanisa makubwa, papa hapa New York, hakuna ushindani miongoni mwao, mnaona, ndugu tu na dada halisi katika Kristo. Nawaambia, hilo lina maana kubwa kwa mchungaji, mwajua. Yote mawili hapa, makanisa ya kale yaliyoimarika hivi, na bado ni ndugu tu na dada, wakifanya kazi kwa ushirikiano. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Hilo ni jema sana. Nafikiri hiyo ni pongezi kwa Ndugu Vick, kwa kazi yake kubwa hapa kwa Bwana, na huruma zake kuu kwa wengine, na wote wawili. Bwana awajalie kuishi muda mrefu, mrefu bado.

³⁹ Pia, Ndugu Vick, nilidhania tulikuwa tunazeeka sana, bali sisi tungali watoto, unaona. Sisi ni watoto tu.

40 Ninamkumbuka Ndugu Bosworth wakati alipokuwa akifa, alikuwa na miaka themanini na minne. Nikasema, karibu niunguze maskini motokaa yangu, kutokana na kufika huko chini ili kumwona. Ndipo nikamwona akisimama, maskini kichwa chake chenye upara, aliinua mikono yake namna hiyo. Niliangukia tu katika mikono yake, na kupiga mayowe, “Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli na wapanda farasi wake!” Ndipo nikasema, “Ndugu Bosworth, ninataka kukuuliza,” nikasema, “je! wewe ni mgonjwa?”

Kasema, “La.”

Nikasema, “Vema, kuna shida gani?”

41 Akasema, “Ninaenda tu Nyumbani.” Naam, mnajua ucheshi wake.

42 Nami ni—nikasema, “Vema, Ndugu Bosworth,” nikasema, “Ningependa kukuuliza jambo fulani. Ni upi uliokuwa wakati wako mzuri kuliko zote?”

Akasema, “Sasa hivi.”

Nami nikasema, “Hata hivyo unajua unakufa?”

43 Akasema, “Siwezi kufa.” Kasema, “Nilikufa yapata miaka sabini iliyopita,” akasema. Akasema, “Mi—mimi ni kiumbe kipya katika Kristo.” Tena akasema, “Ndugu Branham, yote niliyoishia, kwa miaka sitini iliyopita, yamekuwa ni Bwana Yesu. Na, dakika yoyote, ninamtazamia Yeye kuingia mlangoni na kuenda na Yeye kwa ajili ya Umilele.” Nikawaza.

44 Ninamkumbuka Paul Rader. Ni wangapi wanaweza? Wengi wanamkumbuka Paul wakati alipokufa huko nje. Na wao waliita, walikuwa na... Taasisi ya Biblia ya Moody, naamini, walituma ma—maskini kundi la waimbaji wanne kumwambia. Ndipo walikuwa wanaimba *Karibu Zaidi, Na Wewe, Mungu Wangu*, mwajua. Na yeye akasema... Alikuwa na ucheshi, mwajua. Akasema, “Ni nani anayekufa, mimi au nyinyi?” akasema. Akasema, “Sema,” kasema, “inueni hayo mapazia, na mniimbie baadhi, mniimbie wimbo mzuri wa Injili unaochangamsha.”

45 Ndipo wakaanza kuimba, “Chini kwenye msalaba ambapo alifia Mwokozi wangu, chini hapo nililia nitakaswe kutokana na dhambi!”

46 Akasema, “Huo unasikika kuwa bora.” Kasema, “Yu wapi ndugu yangu, Luke?”

47 “Vema, Luke hakutaka kumwona ndugu yake akifa, kwa hiyo alikuwa katika chumba kingine.”

Kasema, “Nendeni mkamwite.”

48 Na Luke na Paul wanasafiri pamoja, kama mimi na mwanangu, Billy Paul husafiri pamoja.

49 Ndipo Luke akaingia, akajaribu kujiimarisha, akashika mkono wa Paul. Paul akanyosha mkono na kumshika, akasema, “Luke, tumetoka mbali pamoja, sivyo, ndugu?”

Akasema, “Naam.”

50 Kasema, “Lakini wazia hilo! Katika dakika tano kuanzia sasa, nitakuwa nimesimama katika Uwepo wa Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake.” Loo, jamani! Hivyo ndivyo.

51 Acha niende namna hiyo. Jambo ndilo hilo, nimevikwa katika haki Yake! Dakika tano kuanzia wakati alipokuwa ameshika mikono ya ndugu yake, “Nitakuwa nimesimama katika Uwepo wa Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake.” Akashika mikono ya ndugu yake kwa nguvu, na akaenda kukutana na Yeye. Loo, jamani, ni siku ya jinsi gani hiyo itakayokuwa, hao askari hodari wa vita!

52 Unaona, ninasimama hapa na kuzungumza na nyinyi, na muda wangu wote umekwisha, nami ninadhani hivyo ndivyo inavyoenenda. Saa tatu, lakini ninaenda kuharakisha, usiku wa leo, hakika kabisa. Ninayo maskini Maandiko machache tu.

53 Mimi huandika chini Maandiko na kujua mahali pa kuyarejea baadaye. Wakati mwingine ninafanya ninii... ninaandika jina, na kisha ninamwuliza Ndugu Vayle kile hilo linachomaanisha, kabla sijaingia, mwajua. Huenda nikalitoa katika Biblia hapa, na yeye ananiambia jinsi ya kulitamka. Na kwa hiyo nimepungukiwa sana katika elimu.

54 Lakini niliahidi usiku wa leo kuwaombea wagonjwa. Na sasa kusudi langu kuu, mi—mikutano yangu, ndiyo sababu sina wakati mwingi sana; mara moja au mara mbili, labda, wakati wa uamsho, nitawaleta watu kama ninavyoenda kufanya usiku wa leo, bila ya upambanuzi, kwa sababu kuwawekea tu wagonjwa mikono. Watu wengi wanaamini hilo. Sasa, hilo, hilo ni—hilo ni jema. Hilo ni Andiko. Unaona? Lakini mnakumbuka, hilo kwa namna fulani lilikuwa ni desturi ya Kiyahudi. Mnaona, Yairo alisema, “Njoo uweke mikono Yako juu ya binti yangu, naye ataishi.”

55 Lakini yule Mrumi alisema, “Sistahili hata Wewe uje chini ya paa langu. Nena tu Neno!” Tazama kile alichoshuhudia. Kasema, “Mimi ni mtu chini ya mamlaka.” Alikuwa ni akida. “Na mimi—mimi ninamwambia mtu huyu, ‘nenda’ na anaenda. Na huyu ‘njoo,’ na anakuja.” Alikuwa anashuhudia nini? Kwamba Neno la Yesu tu lilitosha kumponya mtumishi wake; Yeye alikuwa na mamlaka juu ya magonjwa yote. “Wewe sema tu Neno, mtumishi wangu ataishi.”

56 Aligeuka na kusema, “Sijawahi kupata imani kama hiyo katika Israeli.” Unaona?

Sasa hapo ndipo ninapojaribu kuwafanya watu kuamini.

⁵⁷ Mnajua, watu wengi husema, “Loo, utukufu kwa Mungu, Ndugu *Nanii* aliniwekea mikono, haleluya, nilipona!” Hiyo kwa namna fulani huonekana kama ndugu huyo alikuwa na uhusiano nao. Unaona?

⁵⁸ Sasa kama unaweza tu kutambua Uwepo wa Yesu Kristo, unaona, na kuacha. . . Ni mikono Yake inayojalisha, unaona. Na hebu mkubali tu Yeye, basi hakuna mtu aliyekuwekea mikono ila Kristo. Unaona? Ulimgusa Yeye, na mikono Yake ikakugusa, unaona. Na hakuna mtu anayepata sifa mahali popote. Yote ni sifa. . . Maana, hayo ndiyo yote yanayoweza kufanywa hata hivyo. Kama tukichukua sifa yoyote, tunamnyang'anya Mungu hiyo, kwa sababu Mungu Ndiye ambaye huponya.

⁵⁹ Pia kumbukeni, hakuna kitu kama m—mtu yeyote, awe daktari au mhadumu, ambaye ni mponya. “Mimi ndimi Bwana Mungu wako ayaponyaye magonjwa yako yote,” unaona, “yote.” Hakuna dawa ambayo huponya. Hakuna daktari yeyote ambaye hudai kuwa dawa inaponya. La, la. Dawa husafisha tu huku Mungu anaponya. Dawa haiwezi kujenga tishu, haiwezi kutengeneza mfupa. Unaona? Huenda ukakata na kuondoa kidole tumbo, lakini ni nani anayeenda kuponya mahali kilipotoka, unaona? Huenda ukang'oa jino, lakini ni nani anayeenda kuponya mahali lilipotoka? Unaona? Unaona hilo? Mungu ndiye Mponya, Yeye ndiye Mponya pekee. Maandiko hayasemi uongo. Ni sahihi kabisa, kwa hiyo Yeye ndiye Mponya.

⁶⁰ Ninashukuru sana kwa vi—vitu vyote tulivyo navyo, kama vile dawa wanazoweza kuwazia, zitakazoua viini. Sina chochote dhidi ya hiyo. Ninaomba daima kwa ajili ya hiyo. Lakini tunafikia mahali fulani, hatuna dawa yoyote kusaidia hali hiyo. Na kisha jambo jingine, wakati mwingine, dawa itakayomsaidia mtu mmoja itamwua mwingine. Unaona?

⁶¹ Lakini ninajua Sumu ambayo kabisa si tiba, bali uponyaji, hiyo ni Damu ya Yesu Kristo. Imani katika Damu hiyo!

⁶² Sasa usiku wa leo, loo, sisi, hivi Billy. . . Nilisahau kumwuliza. Niliingia upesi. Je! ali—alisambaza kadi za maombi, je! alisambaza au hakusambaza? [Mtu fulani anasema, “Naam, alisambaza.”—Mh.] Kama hakusambaza, nilikuwa ninaenda kumfanya azisambaze sasa. Tunaenda kuongea tu kidogo kuhusu imani, na halafu—halafu tuende moja kwa moja na kuitisha mstari huu wa maombi, na kuwaombea wagonjwa, kwa kuweka mikono juu yao, kujaribu kupata kila mtu katika jengo tuwezaye kumpata. Sasa, nyinyi iweni na imani sasa.

⁶³ Ninataka mnipe usikivu wenu mkamilifu, kwa dakika chache tu, ninaposoma Neno hili. Na sasa ninataka kusoma kutoka kwa Injili ya Mathayo Mtakatifu, kifungu cha 15. . . mlango wa 15, hasa, kuanzia kifungu cha 21. Na haya si Maandiko mengi kupita kiasi kusoma, mnaona, ni fungu dogo tu. Bali, mnajua, si—si ninii—ninii. . . Si kiasi; ni ubora. Si wingi;

ubora! Unaona, kuna ya kutosha hapo, katika vifungu hivyo vichache hapo, kuokoa ulimwengu mzima. Hakika. Unaona, si—si ukubwa wake, ni kile kilicho.

⁶⁴ Kama nilivyokuwa nikisema hapa wakati fulani uliopita, m—mvulana mdogo, ninaamini ilikuwa ni katika jimbo hili, aliyekuwa akitafuta kwenye dari ya kale na akapata ste—stempu ya kale ya posta. Na—na yeye alimjua mkusanya stempu, kwa hiyo a—akaipoleka ili kuona kuwa ina thamani gani. Naye mkusanya stempu akasema... Loo, bila shaka, mvulana huyo mdogo alikuwa na aiskirimu niani mwake, unajua. Akasema, “Nita—nitakupa dola moja kwa ajili yake.” Vema, jamani, hiyo ilikuwa, uuzaji ulifanywa pale pale. Nafikiri aliiuza kwa yapata, nafikiri, ilikuwa ni mia tano; nayo ikaendelea mpaka, mara ya mwisho tuliposikia, nasahau ilikuwa na thamani ya mia ngapi. Unaona, stempu hiyo ndogo ya kale, karatasi haikuwa ndiyo kitu, ilikuwa tu ni kijipande cha kale cha karatasi ambacho hata hakistahili kuokotwa. Bali ilikuwa ni kile kilichokuwa juu yake, kilichojalisha.

⁶⁵ Hivyo ndivyo ilivyo na Hii hapa. Hiki ni kijipande tu cha karatasi, lakini kile kilicho juu yake ni Neno la Bwana, na hilo ndilo hukifanya kuwa na thamani sana. Vema, kifungu cha 21.

Yesu akaondoka huko, akaenda kando pande za Tiro na Sidoni.

Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo.

Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu.

Akajibu, akasema, Siku—sikutumwa ila kwa...kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.

Naye akaja akamsujudia, akisema, Bwana, unisaidie.

Akajibu akasema, Si vyema kwangu mimi kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.

...akasema, Kweli, Bwana; lakini hata mbwa hula... makombo yaangukayo mezani pa bwana zao.

Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa; na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.

⁶⁶ Sasa kwa dakika chache tu, katika njia ya kufanya... kujenga juu ya hili, ninataka kuchukua fungu kusema yale niliyoandika hapa juu ya Maandiko haya. Ninataka kuita kung’a-... neno *Kung’ang’ania*, na neno moja tu.

⁶⁷ Kung'ang'ania, sasa tunajua neno hilo, nafikiri kwamba linamaanisha “kushikilia,” na kushikilia katika jambo unalofanya. Katika kutengeneza lengo ama kitu fulani, yakubidi kushikilia.

⁶⁸ Na watu kote katika nyakati, ambao wamekuwa na imani katika kile wanachojaribu kutimiza, ilibidi washikilie, hasa ikiwa unajaribu kufanya jambo sahihi. Kwa sababu, unaenda kukutana, unaenda kukutana na upinzani.

⁶⁹ Enyi watu, usiku wa leo, mnaoenda kuombewa, ninasema hili kwa ajili ya utukufu wenu, kwa ufahamu wenu. Ikiwa huko tayari kuja kwenye mstari wa maombi, usije. Kwa sababu, lazima ukumbuke kwamba huu ndio wakati ambapo Mungu anaenda kukuchukua katika neno lake, na wewe inakubidi kumchukua katika Neno Lake. Na haijalishi kile mtu mwingine yeyote asemacho, ama jinsi unavyojisikia, hisia yako haihusiani nayo. Yesu kamwe hakusema, “Je! ulilihisi?” Alisema, “Je! uliamini hilo?” Unaona, huna budi kuamini hilo. Na uponyaji wako tayari umehifadhiwa, Yesu Kristo alikuponya pale Kalvari. Basi, haijalishi shida yako ni nini, huna budi kuukubali. Na kabla hujaweza kuukubali, inakubidi kuuamini. Kwa sababu, imani imewekewa msingi; ama, uponyaji umewekewa msingi juu imani, na imani imewekewa msingi juu ya Neno.

⁷⁰ Sasa, huwezi kusema, “Nikigusa maikrofoni hii, nitapona.” Hakuna, hakuna msingi kwa hilo, unaona. Hilo liko niani mwako.

⁷¹ Bali wakati likiwa ni BWANA ASEMA HIVI, basi unaweza kujua hilo ni kweli, maana, “Mbingu zote na nchi zitapita, bali Neno Lake halitabadilishwa kamwe.” Kwa hiyo ni kweli.

⁷² Sasa inakubidi kung'ang'ania. Haijalishi ni kiasi gani ibilisi anajaribu kukuambia, “Vema, unahisi vibaya tu kama ilivyokuwa.” Kamwe usiamini hata neno lake moja!

⁷³ Hapa wakati fulani uliopita, niliitwa kando ya kitanda, nikatoka kwenye mkutano na kuitwa kando ya kitanda ambapo kulikuwa na m—mvulana mdogo akifa. Na mzee baba yake akanijia, imekuwa yapata miaka kumi na mitano iliyopita, nadhani, ndipo akasema, “Waweza kuja kwa mwanangu, yeye—yeye yuafa kwa ki—kitu cha kuogofya?” Ni u—ugonjwa wa moyo, ninaita... Ninaamini unaitwa namna fulani ya u—ugonjwa wa moyo, ninasahau jina lake sasa, bali ulikuwa mbaya, mbaya kweli.

Na kwa hiyo nikasema, “Naam.”

⁷⁴ Loo, samahani, ulienda kwa moyo wake, bali ulikuwa ni polio iliyokuwa katika mwili wake. Ilikuwa ni polio. Na hiyo ilikuwa kabla hatujawa na chanjo ya Salk. Na basi mvulana huyo alikuwa katika hali mbaya sana. Na kwa hiyo wakati nilipoenda kuomba, daktari asingeniruhusu kuingia. Ndipo akasema, “Siwezi kukuruhusu kuingia.”

⁷⁵ Nami nikasema, “Vema, mimi. . .” Nilikuwa na yapata umri wa miaka arobaini, na nikasema, “Vema, nina umri wa miaka arobaini.” Nikasema mimi. . . “Imani yangu inaniambia kwamba ni sawa kwangu kuenda kumwombea mvulana wa mtu huyu, kwa sababu ananitaka ni—nimwombee.”

⁷⁶ Akasema, “Lakini, angalia,” akasema, “wewe ni mtu uliyEOa. Una mtoto wako mwenyewe. Utaibeba hiyo polio na kumpelekea mvulana huyo.”

Nami nikasema, “Vema, niruhusu niingie.” Asingeniruhusu.

⁷⁷ Na mtu huyo mwenyewe, daktari, kama nilivyofahamu, alikuwa Mkatoliki. Nikasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani. Kama nilikuwa ni kasisi, na mtu huyu alikuwa Mkatoliki, na mvulana huyo alikuwa anakufa, je! ungeniruhusu kuingia kumpa kaida za mwisho.”

Akasema, “Hiyo ni tofauti. Huyo ni kasisi.”

⁷⁸ Nikasema, “La. Ninamaanisha mengi kwao, kama kasisi angamaanisha kwa mtu ambaye ni Mkatoliki.”

Ndipo hatimaye akasema, “Ni ikiwa utatia sahihi karatasi hii.”

⁷⁹ Nikasema, “Nitatia sahihi kitu chochote, unaona.” Na kwa hiyo akanivisha kama Ku-Klux, ndipo ni—nikaingia pale. Sikukusudia kusema hilo namna hiyo; samahani, mnaona; bali, hata hivyo, nyeupe, na kote katika uso wangu.

⁸⁰ Na nikaingia mle ndani, naye mvulana huyo alikuwa chini sana hata alikuwa anapumua kwa shida. Na alikuwa amepoteza fahamu, yapata siku mbili. Na mimi sielewi matibabu na utafiti mkubwa wa kisayansi ambao Mungu amewaruhusu wanadamu kufanya, madaktari kwa ajili ya wagonjwa, na kadhalika, bali kuna namna fulani ya ka—kadiogramu, kitu fulani, kilikuwa kimechukuliwa. Moyo wake ulikuwa chini sana, ninasahau tu kile mdundo ulichokuwa. Ulikuwa karibu umekwisha. Na kwa hiyo mama yake alikuwa amesimama hapo, ndipo nikazungumza na yeye. Kwa hiyo nilienda upande ule mwingine wa kitanda. Naye maskini mwuguzi, loo, msichana anayependeza, yeye, nadhani alikuwa katika miaka yake ya mapema ya ishirini, labda, umri wa miaka ishirini na moja, ishirini na miwili, alikuwa ndiye mwuguzi aliyewekwa kwenye. . . ama alikuwa amtunze huyo mgonjwa.

⁸¹ Na kwa hiyo nilipita nikaenda upande ule mwingine wa kitanda, nikapiga magoti, na nikaninii tu. . . maombi madogo rahisi, na kuweka mikono juu ya—juu ya mvulana huyo. Nikasema, “Bwana Yesu, huyu baba na mama wamenileta hapa kumwombea mwana wao, na yeye yuafa. Na Wewe pekee, Bwana, unaweza kumsaidia. Na mimi ninajua Wewe ulisema, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.’ Ninaomba ahadi hiyo Kwako,

Bwana Yesu, kwa ajili ya uhai wa mvulana huyu.” Hakuna badiliko lililokuja hata kidogo. Nikasema, “Ninakushukuru, Bwana.”

⁸² Ndipo maskini baba huyo akainuka, na kusema, “Bwana, ninakushukuru Wewe sana, shukrani kabisa, kwa kumponya mwana wangu.” Ndipo akanyosha mikono yake na mama akaangukia mikononi mwake, naye akasema, “Baba, wazia hili, anaenda kuwa mzima sasa.” Nami nikasimama na kutazama, na wao walikuwa na furaha na kushangilia, na wakilia. Mvulana huyo alikuwa chini tu alivyoweza kuwa. Wakasema, “Loo, ni ajabu!”

⁸³ Basi maskini mwuguzi huyo akatazama kote, akanitazama mimi. Akasema, “Ni—ninaamini mmelewa visivyo maagizo ya daktari.” Akasema, “Ninaamini mnaelewa visivyo. Mvulana huyu anakufa.”

⁸⁴ “Loo,” mzee huyo akasema, “la, yeye hafi. Anaenda kuishi.”

⁸⁵ Na kwa hiyo yeye akasema, “Tazama, bwana,” kasema, “Ni—ninathamini mtu yeyote kuwa na imani namna hiyo, lakini,” kasema, “unawezaje kucheka na kuendelea namna hiyo,” kasema, “na wewe unaona hakuna tofauti katika mvulana huyu.” Tena kasema, “Mvulana huyu atakufa.” Kasema, “Hawezi kuishi. Vema, hatuelewi jinsi alivyowahi kuishi muda mrefu hivi.” Kasema, “Haijawahi kujulikana katika—katika miongoni mwa watu wagonjwa, ama sayansi, hasa, kwamba mtu aliwahi kushuka chini hivyo akiwa na mdundo wa moyo kama huo,” namna fulani ya kadiogramu, kitu fulani, “aliyewahi kurudi tena.”

⁸⁶ Na mimi kamwe sitamsahau mzee yule. Aliweka mikono yake juu ya bega lake, kama tu baba kwa binti yake, akasema, “Tazama, mpenzi mtoto wangu.” Akasema, “Hiyo kadiogramu ndiyo unayotazama. Hiyo ndiyo uliyofunzwa kutazama. Na hiyo ndiyo yote unayojua habari zake, ni hiyo kadiogramu. Bali,” kasema, “Mimi ninatazama ahadi ya Kiungu.” Unaona?

⁸⁷ Mvulana huyo ameo na anao watoto watatu sasa. Inategemea kile unachotazama. Hakupata nafuu kwa siku mbili au tatu. Lakini baada ya kitambo, kitu cha kwanza unajua, alipona kutokana na huo, na akaenda nyumbani. Yeye ni mmishenari huko Afrika Kusini sasa, akiwa na watoto watatu.

⁸⁸ Sasa, unaona, inaenda tu kuonyesha, inakubidi kushikilia. Hiyo kamwe haikumsumbua mzee huyo. Hiyo ilitosha.

⁸⁹ Sawa tu na wakati yule mwanamke alipoligusa vazi la Yesu Kristo, hilo lilitosha. Ni hayo tu. Yeye, yeye alishikilia mpaka akafika pale, lakini hilo lilitosha.

⁹⁰ Lazima uwe vivyo hivyo. Lazima ushikilie. Na mtu yeyote ambaye amewahi kupata chochote, na kuwahi kufanikisha chochote, amekuwa mwenye kushikilia.

⁹¹ George Washington alishikilia kwenye Bonde la Forge. Matumaini yote yalikuwa kinyume chake, naye a—adui alikuwa ng'ambo ya mto. Lakini baada ya usiku kucha katika maombi; huku askari wa vita wa Marekani wakiwa hawana viatu miguuni mwao, yapata theluthi moja yao walikuwa na viatu, na wakavuka mto kwenye Bonde la Forge, kupitia barafu. Na risasi tatu za gobori zikapitia kwenye koti lake. Bali alikuwa na jibu kutoka kwa Mungu, na hakukuwa na haja kwake kujitoa. Hakuna kitu kingaliweza kumkomesha wakati huo. Alivuka huo kwa sababu aling'ang'ania. Alikuwa amesikia kutoka kwa Mungu.

⁹² Na hivyo ndivyo inavyotupasa kuwa. Mungu akisema hivyo, hilo latosha.

⁹³ Nuhu alishikilia kwa dhati baada ya kusikia kutoka kwa Mungu. Aliposikia Neno la Mungu likimwambia ajenge safina, alijenga. Haijalishi kile mtu yeyote mwingine alisema kuhusu hilo, na jinsi mtu yeyote mwingine alivyowazia kuhusu hilo, Nuhu alishikilia. Huenda walisema, “Vema, yule mzee, ile hadithi ya mvua,” na kadhalika, “maskini jamaa huyo amekaa huko kwenye jua kwa muda mrefu kupita kiasi. Ana kasoro fulani.” Hiyo haikumkomesha hata kidogo. Hakusikia hata neno moja lake. Yeye alisikia tu kwamba Mungu alisema, “inaenda kunyesha; jenga safina,” na yeye alishikilia katika kufanya hilo.

⁹⁴ Sasa, Musa aling'ang'ania kabisa; kwanza, mwoga anayetoroka. Alikuwa amelimika, na, loo, angeweza hata kuwafundisha Wamisri hekima. Alikuwa mwerevu sana, na hata hivyo alishindwa kazini. Ilichukua miaka arobaini kuweka elimu ndani yake, ambayo Farao alimpatia; ilimchukua Mungu miaka arobaini kuiondoa kutoka kwake, kabla Yeye kuweza kumtumia huko nje nyikani. Na wakati mwingine inatubidi kutoa yote yaliyo ndani yetu kabla hujaweza kujazwa. Na sasa alikuwa ameshindwa. Na yeye alikuwa ametoroka na kumwoa msichana huyu mrembo wa Ethiopia, na alikuwa—na alikuwa ametulia na alikuwa na mwana, Gershomu, na alikuwa anaenda kuwa mrithi wa kondoo wa Yethro na kila kitu. Alikuwa ameshau kabisa hisia za watu.

⁹⁵ Bali siku moja, akiwa upande wa nyuma ya jangwa, akitembea kuteremka kwenye njia ya kale aliyoizoea, aliona kichaka kinachowaka moto. Sasa, kamwe hakujaribu kuchunguza kichaka, na kusema, “Ninaamini nitaenda huko na kuchukua majani machache, na kuyapeleka huko chini kwenye maabara na kuona ni nini shida, hata hayateketei. Na ulikuwa umewaka moto hapo kwa saa moja, bali hayo—hayo hayaonekani kuteketea, mti kuteketea.” Iwapo angewazia hayo, Huo usingeongea na yeye. Bali alisogea akiwa na hili moyoni mwake, kwamba angeenda aone. Ndipo Sauti ikasema, “Vua viatu vyako, kwa kuwa uko mahali patakatifu.”

⁹⁶ Ninataka mtambue. Siku moja yeye ni mwoga anayetoroka, na siku inayofuata yeye ni mwe—mwenye msimamao mkali, kesho yake; wakati alikuwa ametoka Misri, wakati alikuwa na jeshi lote mkononi mwake, kuwakomboa watu. Na, unajua, wakati ukisikia sauti ya Mungu, Hiyo hukufanya kutenda mambo ya kigeni, kutenda mambo yasiyoeleweka, ya kipekee na ya namna yake. Sasa wazia tu, yeye ana umri wa miaka themanini sasa, labda ndevu zinaning'inia chini kufikia kiunoni mwake, labda kichwa chake chenye upara kiking'aa, nywele kote shingoni mwake. Naye huyu hapa njiani mwake kuteremka kwenda Misri, akiwa na mke wake ameketi kwa kutagaa juu ya maskini nyumbu, na mtoto kwenye nyonga yake; fimbo iliyopinda mkononi mwake, ameinua macho, akimsifu tu Mungu. Ni tamasha la ajabu jinsi gani!

“Unaenda wapi, Musa?”

“Tunaenda huko chini Misri, kuchukua mamlaka.”

⁹⁷ Uvamizi wa mtu mmoja! Usingeweza kumkomesha. Alishikilia. Kwa nini? Alikuwa amesikia Sauti ya Mungu, hiyo ilitosha kumfanya kushikilia. Mtu mkongwe, mwenye umri wa miaka themanini, alikuwa anaenda kuchukua mamlaka ya taifa, na alifanya hivyo. Alikuwa amesikia Sauti ya Mungu. Anaenda kuchukua mamlaka namna gani, akiwa na hiyo fimbo mkononi mwake? Jeshi lililofunzwa, wanaume milioni moja wamesimama pale, zaidi ya wanaume milioni moja, walikuwa wameshinda ulimwengu katika siku hiyo; na hapa anaenda mtu mkongwe, mwenye umri wa miaka themanini, mke ameketi juu ya nyumbu, na fimbo mkononi mwake, akienda huko chini kuchukua mamlaka ya taifa. Mbona, watu wangeweza kuwazia kwamba alikuwa mwendawazimu.

⁹⁸ Unajua, ukisikia Sauti ya Mungu, na kusikia Neno la Mungu, kwa namna fulani wewe ni mwendawazimu kwa ulimwengu. Lakini ukisikia hiyo Sauti, unajua kile unachofanya.

⁹⁹ Na hakuna kitu kinachoenda kumkomesha Musa basi, alikuwa njiani mwake! Alishikilia kabisa. Hata wakati Farao, alisimama mbele zake, na akatupa chini fimbo na ikageuka kuwa nyoka, nao waganga wakaja na waliweza kufanya jambo lile lile, Musa hakutoroka kama mwoga. Alisimama hapo. Alijua Mungu alimtuma, haijalishi ni waigaji wangapi wa kimwili ambao ibilisi angeweza kuwainua. Alibaki kwenye wajibu wake, maana alikuwa ameisikia Sauti ya Mungu. Alibakia tu hapo na kutazama hao nyoka wakitambaa, na, baada ya kitambo, nyoka wake akaja na kuwala wale wengine. Ni kitu gani kilichofanyikia zile fimbo ambazo nyoka alikula, zilienda wapi? Wazia hilo. Vema.

¹⁰⁰ Daudi, baada ya yeye kumtumainia Mungu, na kumwona Bwana Mungu akiwa pamoja naye, hiyo ilimsaidia kumwua dubu, peke yake, na pia simba. Na ndipo akapata ujasiri,

kwamba Mungu alikuwa pamoja na yeye. Alijua Mungu alikuwa pamoja na yeye, kwa sababu Mungu alikuwa amemfanyia jambo fulani.

¹⁰¹ Mungu amekufanyia jambo fulani. Alikuokoa, huo ndio mwujiza mkuu kuliko yote uliopo.

¹⁰² Sasa Yeye yuko tayari kufanya jambo jingine. Ndipo wakati ukaja ambapo Goliathi alifanya majigambo yake. Mbona, Daudi akasema, “Mnataka kusema kwamba—kwamba mtamwacha huyo Mfilisti asiyetahiriwa asimame hapo na kuyaasi majeshi ya Mungu aliye hai? Mna shida gani nyinyi jamani?”

¹⁰³ Vema, Sauli alikuwa ndiye mtu mwenye uwezo kuliko wote miongoni mwao, kichwa na mabega juu ya jeshi lake. Naye huyu Daudi alikuwa tu maskini mtu aliyedumaa, maskini jamaa mdogo, anayeonekana mwekundu, namna ya m—mvulana, maskini mwenye mabega yaliyoinama, maskini mchungu kondoo. Na kwa hiyo Sauli akasema, “Napenda ujasiri wako, mwanangu. Ila, kumbuka, mtu huyo ni askari wa vita, tangu ujana wake, na wewe si kitu ila kijana.”

¹⁰⁴ Akasema, “Lakini mtumishi wako alikuwa akichunga kondoo wa mtumishi wako, wakati mmoja, ndipo dubu akaja na kunyakua mmoja. Nilimfuata, na Bwana akamtia mikononi mwangu.” Kasema, “Simba alienda, na,” kasema, “nilimwangusha kwa kombeo langu. Ndipo wakati aliposimama, kuningurumia, nilichukua kisu changu, na kumshika ndevuni na kumwua.” Tena kasema, “Ni zaidi vipi Bwana Mungu atamtia huyo Mfilisti asiyetahiriwa mikononi mwangu!” Amina.

¹⁰⁵ Basi ikiwa Mungu aliokoa nafsi yako kutokana na maisha ya dhambi, ni zaidi jinsi gani Yeye anavyoweza kuondoa hiyo kansa!

¹⁰⁶ Mwangelie maskini Daudi. Sauli alisema, “Ninapenda ujasiri wako, lakini wewe si mpiganaji. Lakini ikiwa unataka kuenda, nitakuvisha,” kwa hiyo akavua silaha zake na kumvalisha.

¹⁰⁷ Mbona, maskini Daudi wa kale na hizo Ph.D. zote na D.D.D. zimening’inia juu yake, yeye, mbona, aligundua kwamba fulana ya Sauli ya kikasisi haikumfaa mtu wa Mungu. Kwa hiyo alisema, “Sijawahi kuthibitisha vitu hivi, viondoe kwangu. Niche niende jinsi ninavyotaka kwenda, kwa kile ninachojua ni sahihi.” Loo, jamani! Naye huyu hapa anaenda. Na alishikilia, kwamba angemshinda Goliathi, na alifanya hivyo. Na yeye akamwua Goliathi.

¹⁰⁸ Ninawazia kondoo wake. Hapo alikuwepo Daudi, mtu mwaminifu kwa wajibu wake. Ndipo huyu simba, ambaye angeweza kumwua kwa urahisi, aliingia na kunyakua mmoja wa kondoo wa baba, na akatoka. Na yeye hakuwa na kitu, hasa, cha kupigana na simba, ila kombeo dogo.

¹⁰⁹ Nyinyi wavulana mnajua. Ni mara ngapi imenibidi kulipia dirisha! Na kijipande kidogo cha ngozi, na kamba, unajua, na kushindilia jiwe hili na kulitupa kwa kombeo. Na sisi tulikuwa tukiwapiga hawa madaktari wa nyoka kutoka kwenye uzio, na kadhalika, na—na kurusha kwa haya makombeo.

¹¹⁰ Hayo ndiyo yote aliyokuwa nayo Daudi; ingekuwa vigumu hata kumwua sungura. Lakini tunaona kwamba Daudi, chochote alichokuwa nacho mkononi mwake, hakikuwa kikubwa sana, bali alikuwa na ujasiri. Naye alijua huyo alikuwa ni kondoo wa baba. Na yeye alikuwa—alikuwa ametumwa huko nje, na baba, kuwachunga kondoo hawa. Aliwawajibikia. Na sasa alichukua chochote alichokuwa nacho mkononi mwake, na akaondoka kwenda kumrudisha huyo kondoo, akishikilia, ili aweze kumchukua kutoka kwa huyo simba.

¹¹¹ Hivi mliwahi kumwona simba, jinsi anavyofanana? Mmewaona hawa walioko kizimbani; vema, hao ni—hao ni watoto. Mnapaswa kumsikia mmoja mwituni. Jamaa hawa hapa, wamekuwa kizimbani na kifungoni; ukisikia mmoja wao akinguruma, inatoa sauti mbaya. Unapaswa kumsikia mmoja huko nje mwituni, ukimwinda, na unajua kwamba yeye anakuwinda, pia. Ndipo, loo, jamani, yeye ni jamaa mkubwa! Akinguruma; mende, tumbili, nyani, na mbwa mwitu, kila kitu kinasimama. Yeye ni mfalme, nao wanampa nafasi.

¹¹² Lakini hapa Daudi anaenda na maskini kombeo hili, kurudisha kondoo yule, na alimrudisha.

¹¹³ Loo, jamani, jinsi ambavyo ningechukua somo juu ya hilo kwa dakika chache. Naam, bwana. Wewe ndiwe kondoo wa Mungu, pia. Ugonjwa umekushika. Sina mengi sana, si—si hata kombeo, bali niko na Neno. Ninakufuata, usiku wa leo, kukurudisha. Ninakuja kukuokoa, na Neno la Bwana. Sijui chochote kuhusu dawa na kukata kwa visu, na kadhalika, ila *Hili* nimethibitisha. Ninajua kwamba Hili ni kweli, kwa hiyo ninakufuata wewe kondoo, kukurudisha kwenye malisho ya majani mabichi ya upendo wa Mungu tena. Mungu, nisaidie pamoja na maskini kombeo hili.

¹¹⁴ Daudi alikuwa amelifunika katika—katika vidole vyake, na alikuwa na mawe matano mkononi mwake. Ni nini hayo? I-m-a-n-i katika J-e-s-u-s. Na yeye hapa anakuja, na yeye alirudisha kondoo.

¹¹⁵ Sasa hivyo ndivyo tunavyofanya usiku wa leo, tukiwa na imani katika Yesu, na kwa kung'ang'ania tunaenda kusimama juu ya Neno Lake lisiloguswa. Na sisi tunaamini kwamba Mungu atatimiza Neno Lake. Hilo lisipotimia, basi sote tumepotea. Kila Neno la Mungu linaitikiwa na “amina,” kwa mwaminio. Hiyo ni kweli. Naam, yeye alishikilia.

¹¹⁶ Na pia Samsoni, wakati alipokutana na wale Wafilisti, je! uliwahi kuwazia hilo? Mbona, Samsoni, wamechora picha

yake kama mtu aliye na mabega kama milango ya ghala. Vema, isingekuwa si—siri yoyote, kumpata mtu kama huyo, angeweza kunyakua simba na kumrarua vipande viwili. Lakini Samsoni alikuwa... Samahani kwa tamshi hili, nitalifanya tu kama kwamba alikuwa ni maskini kibushuti mwenye nywele za kipilipili, mvulana mdogo tu wa mama, vishungi saba vinavyoonekana vya kidondoadume vimening'inia chini. Unaona? Kitu gani, pia kumbukeni, yeye alikuwa ni mnyonge mpaka Roho wa Bwana alipokuja juu yake, ndipo akamchukua simba na kumrarua vipande. Hiyo ni kweli. Kwanza, Roho wa Bwana juu yake, ndipo akajua mahali alipokuwa amesimama.

¹¹⁷ Na iwapo kanisa linaweza tu kutiwa upako, kupakwa na imani halisi. Wakati huyo simba aliponguruma, nadhani Samsoni alitetemeka. Lakini Roho wa Bwana alikuja juu yake. Alishikilia, akasema, “Niko tayari kukutana na wewe,” akamnyakua huyo simba, akamrarua vipande na kumtupa kando, na kuendelea kutembea.

¹¹⁸ Walimzingira, usiku mmoja. Pia alichukua malango ya Gaza, akayaweka juu ya mabega yake, na akatembea kwenda nayo juu ya kilima. Jamani, loo, jamani, ni mtu wa namna gani, maskini kibushuti kama huyo. Bali, jambo lilikuwa kwamba, Roho wa Bwana alikuwa juu yake. Alikuwa. Hilo ndilo lililoleta tofauti.

¹¹⁹ Ndipo siku moja, alizungukwa na Wafilisti elfu moja. Naye huyo hapo, hakukuwa na chochote alichokuwa nacho, kwa hiyo akachukua mfupa wa taya la nyumbu, labda alikuwa amekufa kwa miaka arobaini au zaidi, na ulikuwa ni maskini mfupa mkavu kwelikweli. Na hao Wafilisti walikuwa wamevaa kofia za chuma, na makoti ya kile wanachokiita deraya, ambayo ni vipande vikubwa vinene vya chuma au shaba, na kofia ya chuma yapata unene wa inchi moja. Na yeye alichukua huo mfupa wa taya la huyo nyumbu, na kuwaua Wafilisti elfu moja.

¹²⁰ Hivi uliwahi kuwazia? Chukua maskini mfupa huo mkavu wa taya kutoka jangwani kule, na kupiga moja ya hizo kofia za chuma, mbona, mfupa huo wa taya ungevunjika vipande elfu moja. Lakini alisimama hapo, na kupitia hizo helmeti za chuma, wao wakiwa na mikuki, aliwapiga tu kulia na kushoto, mpaka akawapiga na kuwaangusha elfu moja. Wale waliobaki walikimbia wakapanda kwenye miamba.

¹²¹ Ilikuwa ni kitu gani? Mradi tu aliweza kunyosha mkono pale nyuma na kugusa hivyo vishungi saba, hivyo vilikuwa ni agano la Mungu. Hakukuwa na chochote kilichokuwa kinaenda kumsumbua mradi tu alikuwa na ahadi hiyo ya agano.

¹²² Wala hakuna chochote kiwezacho kulihangaisha Kanisa la Mungu aliye hai mradi tu tunaweza kuhisi huyo Roho Mtakatifu, agano la Neno la Mungu ndani ya mioyo yetu, Baraka ya Kipentekoste. “Kwa kuwa kazi nizifanyazo Mimi, mtazifanya pia. Uhai ulio ndani Yangu, utakuwa ndani yenu. Kama Baba

alivyonituma Mimi, ndivyo nami ninavyowatuma.” Yule Baba aliyemtuma, alikuja ndani Yake. Yesu yule anayemtuma mtu, huenda ndani ya mtu huyo. Si mtu huyo; ni Yesu. Haikuwa Yesu; ilikuwa ni Mungu. “Kama Baba alivyonituma, ndivyo nami ninavyowatuma. Tazama, niko pamoja nanyi daima, hadi ukamilifu. Nitakuwa pamoja nanyi, hadi mwisho wa ulimwengu. Na kazi nizifanyazo, nanyi pia mtazifanya. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena; hata hivyo nyinyi mtaniona, mwaminio, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu,” Yesu Kristo. Mradi tu ninaweza kuhisi huyo Roho wa Mungu karibu, jambo fulani linaenda kutendeka. Ninaweza kuona watu ambao wataamini Hilo, ambao wataakisi sifa na Utukufu wa Mungu.

¹²³ Kila wakati unapoangalia mwezi, si mwezi unaoangaza, ni jua linaloangaza juu ya mwezi. Kama ningeweza kusema, “Mwezi, ni kitu gani kinachokufanya kuangaza?” Sema, “Si mimi ninayeangaza. Ni kitu fulani kinaangaza juu yangu. Ninapaswa kudumisha nuru kuendelea, wakati jua halipo.”

¹²⁴ Nalo Kanisa ni mfano wa mwezi. Tunapaswa kuakisi Nuru wakati ambapo Mwana wa Mungu hayupo, maana sisi ni wana na binti za Mungu, Nuru ndogo, na mradi tu tunaweza kuuona huo mwezi unaakisi aina ile ile ya Nuru ambayo jua huangaza. Loo, sio—sio watu, ni Mungu ndani ya watu.

¹²⁵ Nilikuwa, wakati nilipokuwa, nilikuwa bwana nyama kwa miaka kadhaa. Ninapenda wanyama, na ni—ninapenda kuwatunza. Kwa hiyo ni—nilikuwa afisa wa uhifadhi kwa miaka saba. Nilikuwa nikipitia karibu na chemchemi ya kale. Hiyo ilikuwa ndiyo chemchemi nzuri kuliko zote niliyowahi kunywea. Ilikuwa...Daima niliipenda kwa sababu ilikuwa na furaha, daima ikibubujika, kububujika tu, kububujika, kububujika. Nami nikawaza, “Jamani!” Ninaketi chini na kunywa. Siku moja, niliwaza, “Maskini chemchemi, ni kitu gani kinachokufanya kuwa na furaha sana? Je! ni kwa sababu sungura wanakunywa kutoka kwako?”

¹²⁶ Kama angeweza kuzungumza, angesema, “La, hilo silo linalonifanya kububujika.”

¹²⁷ Nami ningesema, “Labda kulungu hunywa kutoka kwako, mara moja moja.”

“La, hilo silo linalonifanya kububujika.”

¹²⁸ “Vema,” ninasema, “maskini chemchemi, labda ni kwa sababu mimi hunywa kutoka kwako, yapata mara moja kwa mwezi.”

¹²⁹ Kasema, “La, hilo silo.” Ningesema, “Vema, ni kitu gani kinachokufanya kububujika namna hiyo wakati wote?”

¹³⁰ Kama angeweza kuzungumza, angesema, “Si mimi ninayebubujika. Ni kitu fulani nyuma yangu, kinachonifanya kububujika. Kinabubujika.”

¹³¹ Na hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo kwa mwaminio. Kuna kitu nyuma yako. Huwezi kusukuma Hicho, kurarua Hicho. Hicho hukutunza. Hicho Ndicho hufanya mbubujiko, Kitu fulani ndani yako. Kama Yesu alivyomwambia yule mwanamke kisimani, “Kisima cha maji kinachobubujika hadi Uzima wa milele,” mabubujiko tu ya kawaida yakirusha juu furaha za Mungu kupitia nafsi yako, wakati wote. Na mradi tu Kanisa lingeweza kuhisi hilo karibu nao, una—unatishwa na nini, unaona?

¹³² Samsoni hakuogopa. Alishikilia. Yote aliyokuwa nayo ulikuwa ni m—mfupa wa taya la nyumbu, bali alishikilia kwa sababu alijua vishungi vyake vingali vilining’inia pale.

¹³³ Daktari huenda amekuambia, “Hakuna nafasi kwako kupona. Unakufa. Uko na kansa.” Bali mradi tu unaweza kuketi hapa na kuhisi ufufuo mtukufu wa Yesu Kristo, inaleta tofauti gani kile daktari asemacho sasa inaleta tofauti yoyote? Unaona, wewe shikilia. Angekuthamini kama yeye ni daktari mzuri, angekuambia kwamba anataka uwe mzima. Hilo ndilo—hilo ndilo analotaka ufanye. Na huna budi kulifanya; kuwa na imani, lazima ushikilie.

¹³⁴ Yohana alikuwa na hakika kabisa kwamba angeona ishara sahihi! A—alijua Mungu alimwambia angejua ni Nani aliye Masihi. Alishikilia kabisa!

¹³⁵ Na mtu fulani huenda alisema, “Vema, hivi hufikiri kwamba huyu Ndiye?”

¹³⁶ Akasema, “Nitamjua Yeye atakapokuja.” Alikuwa na hakika kabisa, hata alisema, “*Huyu* ndiye Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu.” Alijua ilikuwa. Alishuhudia hilo. “Niliona Roho wa Mungu akishuka kutoka Mbinguni juu Yake, kama hua, na mimi ninajua huyo ni Mwana wa Mungu.” Kushikilia! Loo, tungeweza kuendelea na kuendelea, na wahusika.

¹³⁷ Maskini mwanamke huyu, alikuwa ni Myunani kutoka nchi ya Sirofoinike, na tunaona kwamba hapana shaka alikuwa amesikia kuhusu sifa na utukufu wa Bwana Yesu. “Imani huja kwa kusikia, kusikia Neno la Mungu.” Alisikia, na wakati aliposikia...

¹³⁸ Unajua, imani hupata vyanzo vyake ambavyo wengine hawaoni. Sasa ikiwa huna imani, vema, basi, hakuna haja ya kujaribu kukuonyesha hiyo. Kwa sababu, imani inaweza kuiona. “Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.” Imani huona kile ambacho watu walio vipofu hawaoni. Imani ndiyo hisi ya sita. Hisi tano ni nzuri, mradi tu hazikosi kukubaliana na ya sita. Bali hisi ya sita ni

imani, “ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo,” huoni, kuonja, kugusa, kunusa, au kusikia, bali hata hivyo unajua. Imani inakwambia hivyo. Na ni hakika kabisa kwamba ni halisi, kwamba inakuja kwako kitu halisi. Sio tu mawazo. Ni kitu ulicho nacho.

¹³⁹ Ninawaona watu wakija jukwaani, kasema, “Ndugu Branham, ninayo imani yote!”

“Vema, unafanya nini hapa juu, basi?” Unaona? Unaona? Unaona?

¹⁴⁰ “Sina hiyo.” Na, lakini hapo ukipata, wakati kitu chochote...

¹⁴¹ Umekuwa na mambo yakitendeka, ulijua tu yalikuwa yanaenda kutendeka. Hata hivyo hukujua jinsi yalivyokuwa yanaenda kuwa, bali yalikuwa yanaenda kuwepo. Hiyo, hiyo ni imani. Hiyo ni imani halisi. Yanaenda kufanyika basi, wakati unajua kuwa yanaenda kuwepo. Sasa, imani hupata chanzo ambacho wengine hawaoni.

¹⁴² Neno Lake ni upanga. Biblia ilisema hivyo, katika Waebrania 4:12, kwamba Hilo ni upanga. Bali inahitaji mkono wa imani kuutumia upanga huo. Imani ndiyo pekee inayoweza kufanya hilo, kushika upanga.

¹⁴³ Alikuwa na vizuizi vingi, maskini mwanamke huyu. Sasa, alikuwa na binti ambaye alikuwa—alikuwa na kifafa, na yeye alikuwa katika hali mbaya, mbaya sana. Na yeye alikuwa amesikia kwamba Yesu aliponya kifafa. Sasa, “imani huja kwa kusikia,” na huyo alikuwa ni mtoto wake, kwa hiyo alikusudia ku—kuketi chini mahali fulani na kumsikia Yesu. Na sasa alikuwa na vizuizi vingi, vingi kabisa, vizuizi vingi, lakini imani yake haikuwa na kizuizi chochote.

¹⁴⁴ Usiku wa leo, watu wana vizuizi vingi. Ikiwa wewe... Nia yako ina vizuizi vingi sana. Bali, imani yako, hakuna kitu kinachoweza kusimama njiani mwake. Imani haijui kizuizi chochote.

¹⁴⁵ Hebu tuwazie tu baadhi ya mambo ambayo huenda yalimfanyikia maskini mwanamke huyu. Huenda walimwambia, kwamba, “Wewe ni Myunani.” Kwa maneno mengine, “Dhehebu lako halidhamini mkutano ule kule chini. Huna haki yoyote kwenda huko chini.” Vema, kama hilo lingekuwa niani mwake, asingaliketi muda mrefu hata hivyo. Yeye, jagi ingalijaa, na yeye angaliondoka. Lakini tunaona, hilo halikumkomesha. Kama alikuwa Myunani au sivyo, yeye alikuwa na imani. Hayo ndiyo yote aliyohitaji ilikuwa ni imani.

¹⁴⁶ Sasa mtu fulani huenda alimjia, na kusema, “Vema, siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho. Watu hao ni kundi tu la—la walokole.” Lakini bado alishikilia. Alikuwa anaenda kuenda hata hivyo.

¹⁴⁷ Hebu tuwazie jingine. Baadhi yao huenda walisema, “Vema, unajua nini, mume wako ni m—mtu maarufu hapa mjini, na kama ungepatikana huko chini pamoja na lile kundi, vema, mume wako kwa kweli atakuacha.” Lakini bado alishikilia. Alikuwa na imani, na alikuwa na haja kuitumia.

¹⁴⁸ Baadhi yao huenda walisema, “Mbona, kama ungeteremka kwenda kwenye mchezo wa karata, ama aina yoyote ile ya burudani ambayo wewe huenda, watu watakucheka.” Bado alishikilia.

¹⁴⁹ Ndipo basi labda kitu kile cha kale huenda kilimjia, “Unajua, mchungaji atakufukuza kanisani ukienda huko chini na kuchangamana katika kitu kama hicho.” Lakini hilo halikumkomesha. Alikuwa angali ameshikilia. Alikuwa anaenda hata hivyo. Kwa nini? Alikuwa ameigonga imani. Imani inaenda kulifanya. Sijali kile watu wengine wanachofikiria; imani huifanya.

¹⁵⁰ Hatimaye, alipenya kupitia vizuizi hivi vyote, na akamfikia Yesu. Sasa, inaonekana, shida zake zote ziliisha, alimfikia Yesu; bali, haikuwa hivyo, zilikuwa tu zimeanza.

¹⁵¹ Watu wengi wangesema, “Vema, kama ninamjua Yesu. . .” Naam, tunaona hayo kila usiku. Unaona, Yeye huja moja kwa moja pamoja na sisi, kila usiku, hujithibitisha Mwenyewe kuwa hapa, lakini hata hivyo tunarudi usiku unaofuata, pamoja na shida zetu zote tena, unaona. Unaona? Hiyo ni kweli? Sasa hiyo ni kweli.

¹⁵² Alifika kwa Yesu. Yeye atakuwa pengine labda. . . Kama hakuwa na imani ya namna hiyo, kitu cha kwanza cha kuvunja moyo baada ya kumpata Yesu, mbona, angekuwa. . . angelipuka, na kurudi. Bali, unaona, imani haitafanya hivyo. Imani haitaachilia. Imani hushikilia. Inashikilia moja kwa moja. Sasa angalia, mwanamke huyo alikuwa na ujasiri na imani katika Mtu huyu. Sasa kama alikuwa tu akidhihaki, ama kusema tu, “Ninateremka huko chini na kulijaribu, nitaona kile Yeye anachosema. Kama Yeye akisema jambo dhidi ya kanuni zetu za imani, tuta—tutaondoka tu. Hayo tu.” Lakini yeye alikuja kupata kitu fulani, na alikusudia kuketi hapo mpaka akipate. Haya basi, huyo ndiye mtu; kama vile malkia wa Kusini, tuliyehubiri juu yake hivi majuzi usiku.

¹⁵³ Angalia wakati alipomfikia Yesu. Badala ya kupata karibisho, alipata kukataliwa. Sasa wakati wewe. . . Unafikiri nini kuhusu watu leo hii wangepikia mahali hapo na kutendewa namna hiyo? Yesu alimwambia upesi sana. Baada ya yeye kupitia vizuizi hivi vyote, na hatimaye. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] akasema. . .

¹⁵⁴ Yeye alikuja Kwake. Na alikimbia mpaka Kwake, kumwabudu Yeye, ndipo kasema, “Ewe Mwana wa Daudi, nirehemu, binti yangu amepagawa sana na ibilisi. Na mimi

nimejua kwamba Wewe ni Mponyaji mkuu, na nimekuja ku—kukuomba Wewe unisaidie.” Alimpuuza tu. Alimtaazama, akaendelea kutembea. Loo, jamani! Alikuwa kidogo zaidi ya Pentekoste yetu ya kisasa; jamani, wangeinua pua yao na kurudi nyuma, kasema, “Hainipasi kufanya hivyo.” Lakini si yule mwanamke. Yeye alikuwa na imani. Alikaa pale pale.

¹⁵⁵ Sasa huyo mwanamke alimfuata Yeye tena, “Bwana, siwezi tu kupata?” Na yeye hakuwa akiwazia yale aliyokuwa amepitia. Hakuwa akiwazia yale ambayo ingembidi kupitia. Jambo pekee alilojua, aliamini kama angeweza kumfanya Yeye asema hivyo! Hayo tu ndiyo aliyohitaji kujua, kama Yeye angesema hivyo! Alijua ilikuwa inafanya kazi juu ya wengine, kwa nini isifanye kazi juu yake?

¹⁵⁶ Unapiga vita kila inchi ya safari. Mungu, huko chini Misri, aliwapa Wayahudi Palestina, bali walipiga vita kila inchi ya safari! Mungu alimwambia Yoshua, “Kila mahali nyayo za miguu yenu zinapokanyaga, hapo nimewapa.” Nyayo za miguu zilimaanisha ushindi, umiliki, na umbali tu unavyoweza kupanda katika Ufalme wa Mungu. Kama unataka tu kupanda mahali padogo, na kusema, “Vema, ninaamini huenda haitanibidi kuenda kuzimu, bali ninaamini kuwa nitaokoka hapo mwisho, nikijiunga na kanisa,” huna msingi wa kutosha bado. Bali kila ahadi katika Biblia ni yako, ila itakubidi kumpiga vita kila ibilisi mlinzi atoke kwake, kwa upanga ukatao kuwili, na kuidai kwa ajili yako. Shikilia, ukiingia moja kwa moja ndani yake.

¹⁵⁷ Sasa alifika moja kwa moja kwa Mungu Mwenyewe. Na Yeye akampuuza. Ndipo akakimbia kumfuata Yeye, akilia. Alishikilia. “Bwana, nisaidie,” akasema. Alimwabudu Yeye, kasema, “Nisaidie!”

Sikiliza kemeo hilo. “Mimi sijatumwa kwa jamii yenu.” Loo, jamani!

¹⁵⁸ Basi wengi wao wangesimama, kasema, “Vema, nafikiri Yeye hakutumwa kwetu. Uamsho huu sio. Nafikiri nitaondoka.”

Unaona, Yesu alijua alikuwa na aina hiyo ya imani. Unaona?

¹⁵⁹ Na jambo jingine Yeye alilosema, “Jamii yako ni kundi tu la mbwa.” Whiu! Jamani!

¹⁶⁰ Usiwazungumzie hivyo Wapentekoste mamboleo. Loo! Unasema hilo, wanasema, “Vema, nitaliacha tu kundi hili na niende nijiunge na Assemblies. Na Assemblies wakiniambia, nitaenda kwa wengine, na wengine, na wengine, unaona.”

Bali si mwanamke huyo. Yeye alikuwa na imani.

¹⁶¹ Kasema, “Ninii yako . . . Sikutumwa kwenu. Sikutumwa kwa jamii yenu. Na, mbali na hayo, nyinyi si kitu ila kundi la mbwa. Si vizuri Mimi kuchukua chakula cha watoto hapa, na kuwatupieni nyinyi kundi la mbwa.” Loo, jamani!

¹⁶² Hiyo haikomeshi imani. Imani ingalipo, mpya tu kama ilivyowahi kuwa. Imani hukubali nini? Kweli. Alisema, “Hiyo ni kweli, Bwana.” Loo, jamani! Ona jinsi unavyoweza kuwa mdogo, si jinsi unavyoweza kuwa mkubwa. Imani hukufanya mdogo. Angalia, angali aling’ang’ania.

¹⁶³ Hata hivyo, Yeye asingeweza kumsikiliza huyo mwanamke. Alimpuuza. Basi hatimaye aliingia katika njia Yake na Yeye asingeweza kumwepuka, na ndipo Yeye akamwambia, kasema, “Sijatumwa kwenu, na ninii yenu. . . kwa jamii yenu. Na jamii yenu si kitu ila kundi la mbwa. Na mimi sitachukua chakula cha watoto. Si vizuri mimi kuchukua chakula cha watoto, uponyaji kwa kundi hili, na kuwapa nyinyi mbwa.”

Ndipo yeye akasema, “Hiyo ni kweli, Bwana.”

¹⁶⁴ Imani daima itakubali kuwa Neno ni Kweli. Amina. Unaona? Ikiwa una imani halisi, na Biblia inakuambia kwamba unafanya kosa, utakubali kwamba uko makosani. Hutasema, “Sasa, ngoja kidogo hapa, mimi ni mfuasi wa. . .” La, la, hiyo siyo imani. Neno likisema hilo, kwamba wewe. . . Hapo ndipo ulipo sahihi au makosani, ni kwa Neno. Hiyo ni kweli.

¹⁶⁵ Sasa yeye alisema. La, bwana, hilo, asingeweza tu kuamini kwamba angeweza kusimama katika hilo, kwa hiyo anaondoka anaenda. Ndipo akasema, “Kweli, Bwana, sisi si kitu ila mbwa, bali ninaomba tu kwamba niweze tu kupata baadhi ya makombo yanayoanguka kutoka kwenye meza ya Bwana.” Alikuwa anatafuta makombo. Wazia tu hilo.

¹⁶⁶ Leo hii, ama tupate boflo nzima au hatutachukua wowote hata kidogo. Unaona? Inatubidi kuwa wote wa hiyo au hatuchukui chochote.

¹⁶⁷ Angali alishikilia. Aliendelea moja kwa moja. Yeye hakuwa mmea wa tuta maalum ambao ilibidi kubembelezwa na kuninyiziwa, kuondoa mchwa. La, bwana. Yeye hakuwa mmoja wa hizo mbegu zilizochanganywa kama mmea wa kisasa wa leo hii, wanaojiita Wakristo. Wakati Neno la Mungu liliposema hilo, na yeye akaliadini, aliliona limethibitishwa, alikuwa tayari kulifuata haidhuru ni nini mtu yeyote alisema. Hata Kristo Mwenyewe asingeweza kumkomesha. Hilo ndilo imani hufanya. Loo, hiyo hukubali Neno kuwa sahihi. Alikuwa akitafuta makombo.

¹⁶⁸ Kumbukeni, alikuwa hajawahi kuona mwujiza. Alitoka katika dhehebu ambalo halikuamini miujiza. Yeye, akiamini, ilibidi atoke katika dhehebu lililosema, “Hakuna kitu kama miujiza.” Yeye alikuwa ni Mtaifa. Hakuwa amewahi kuona mwujiza, maishani mwake. Lakini hata hivyo, imani ikishika, Mungu yupo hapo. Unaona? Hakuwa amewahi kuuona, lakini alikuwa amesikia habari zake.

¹⁶⁹ Ikiwa huamini kwamba kuna miujiza, soma Biblia na ahadi zake kwetu leo hii. Imani ilishika.

170 Alikuwa kitu kama Rahabu kahaba. Wakati aliposikia, kwa wapelelezi, hakutaka kumwona Yoshua, na kuona jinsi alivyovalia na namna ya askari wa vita aliyokuwa. Akasema, “Nimesikia kwamba Mungu yuko pamoja nanyi. Nimesikia yale Mungu aliyofanya.” Na yeye alitaka wokovu, na aliupata; kweli, kwa sababu alishikilia, pia. Alisema, “Nitawaficha. Nitafanya chochote. Lakini jambo moja ninalotaka mniapie, kwamba nitaokolewa kwenye wakati huu.” Loo, jamani, hilo ndilo wazo.

171 Basi maskini mwanamke huyu alikuwa hivyo. A—alitaka, alijua kwamba alikuwa anaenda kuupata. Hakukuwa na shaka. Haijalishi kile kilichombidi kupanda kupitia, alikuwa anaenda kuupata kwa vyovyote vile. Kwa hiyo Yesu asingeweza hata kumfanya arudi nyuma, kwa kumwita wa jamii isiyofaa, kumwita mbwa, “Haikuwa sahihi kuchukua chakula cha watoto na kuwalisha mbwa,” na kadhalika namna hiyo. Lakini bado aliufuatilia moja kwa moja, hata hivyo, kwa sababu alishikilia. Alikuwa na haja, binti yake alikuwa anakufa. Wengine walikuwa wameponywa, basi ni kwa nini binti yake asiweze kuponywa? Na huyo alikuwa ni Mungu wa uumbaji.

172 Yesu alisema, “Kwa tamko hili, ibilisi amemwacha binti yako.” Loo, jamani! Aliiendea karama ya Mungu kwa njia sahihi.

173 Je! unajua Mungu hufanya mambo wakati mwingine ili tu ku—kufanya mambo kwa njia tofauti, na ili tu kuona kile ambacho watu watafanya? Sasa liko juu ya kichwa chako, hamjaliona wala hamjalitambua, bali nimefanya jambo fulani sasa hivi ili tu kufanya jambo. Na hilo limenisaidia sana. Nami nililiona likifanya kazi. Unaona, unasema mambo, unabadilisha mtazamo wa—wa—wako, unabadilisha sauti yako, unabadilisha wakati mwingine mahubiri yako; kuangalia na kuona mambo fulani, halafu kuangalia na kuona jinsi linavyofanya. Kwa sababu, mstari wa maombi unakaribia kuja, ingekuwa bora hilo lisiweko miongoni mwenu. Mnaona? Unaona, kuliona tu likitendeka, halafu unageuka mwenyewe na kurudi nyuma mahali pengine tena. Unaona? Mungu alifanya jambo lilo hilo. Angali analifanya, kutambua.

174 Aliiendea karama ya Mungu kwa njia sahihi. Pia kumbuka, yeye alikuwa ndiye wa kwanza, Mtaifa, ambaye Mungu aliwahi kufanya mwujiza juu yake. Alikuwa ndiye Mtaifa wa kwanza.

175 Imani hukubali Neno ni Kweli. Nayo ina kicho, ina kicho sana, na hiyo ndiyo, na ng’ang’anifu, na hiyo ndiyo iliyo.

176 Martha, wakati alipoenda kukutana na Yesu. Sasa iwapo kuna yeyote aliyekuwa na haki ya kukemea, ingekuwa ni Martha, maana alikuwa amemwita Yesu aje amwombee ndugu yake wakati alipokuwa mahututi, akifa, naye Yesu. . . Walikuwa wameacha kanisa, walikuwa wametoka kwenye huduma ya kale iliyokufa waliyokuwa ndani yake, na walikuwa wamemfuata

Bwana Yesu, wakimwamini Yeye kuwa ndiye Masihi mpakwa mafuta. Ndipo basi rafiki Yake mwenyewe, Lazaro, ambaye Yeye alikua pamoja naye. . . Na wao walikuwa wametengwa kutoka kwa kanisa lao na kutoka kwa shirika. Na rafiki Yake mwenyewe ambaye Yeye alikua pamoja naye, alikuwa amelala mgonjwa, katika hali ya kufa. Daktari asingeweza kumsaidia.

¹⁷⁷ Ndipo yeye akamwita Yesu, na Yesu kwa urahisi alipuuza tu wito wake. Ndipo Yeye akaenda kwenye mji mwingine, na Yeye akafanya jambo lilo hilo huko. Wakaita tena, na Yeye akapuuza tu na kuendelea.

¹⁷⁸ Ndipo basi baada ya Lazaro kufa, na alikuwa amezikwa siku nne. Uso wake tayari ulikuwa umebonyea, kufikia wakati huo, nchi hiyo yenye joto. Pua huanguka kwanza, kama ninavyoambiwa, na labda mwili wake ulikuwa tayari umebonyea. Kwa sababu, baada ya saa sabini na mbili, uharibifu huingia katika mwili, na kwa hiyo tunaona.

¹⁷⁹ Ninapaswa kumzika mtu katika siku chache, Jumatano. Na yeye alikufa Jumatano iliopita, na wao walimfungia tu, na wananingojea tu mimi huko nije nihubiri mazishi yake. Labda wasingeweza kumweka nje zaidi, kwa sababu u—uso wake ungebonyea. Unaona?

¹⁸⁰ Na hilo ndilo lililokuwa linamfanyikia Lazaro. Alikuwa tayari amekufa.

¹⁸¹ Na ndipo baada ya yeye kufa, na ilikuwa imekwisha, basi hapa akaja Yesu akiingia mjini kwa siri. Kwa hiyo basi walijua walikuwa wanaenda kukosolewa, kwa sababu labda tayari walikuwa wamekosolewa.

¹⁸² Lakini Martha, alikuwa amechelewa sana, inaonekana; kuhusu kumwandalia Yesu mahali pa kulala, mahali kwa ajili Yake kula, na kadhalika. Hata alimwomba Yesu, wakati mmoja, kumfanya dada yake kuja kumsaidia. Lakini chini katika moyo wake, imani iliingia. Huku Mariamu amekaa kimya, akilia, bila kufanya chochote juu yake, na kukata tamaa; Martha anatoka kisiri kutoka kwenye—kutoka kwenye nyumba, na kuteremka kupitia mjini. Hapana shaka, alikutana na wengine mtamani, kasema, “Yuko wapi yule mponyaji wa Kiungu mliyekuwa naye hapa? Vipi kuhusu Lazaro sasa?” Yeye aliwapita tu na kuendelea.

¹⁸³ Alifikia mahali Yeye alipokuwa. Angalia jinsi alivyokuwa. Alikimbia kuenda Kwake. Alikuwa na haki ya kumkemea, alikuwa na haki ya kumwambia, akisema, “Sasa kwa nini Wewe hukuja wakati nilipokuita?” Kama huyo angalikuwa M—Mpentekoste wa leo hii, ama Mbaptisti, au Mpresbiteri, wangebadiisha makanisa upesi sana. Unaona? Hakika. “Kwa nini Wewe hukuja wakati tulikuita?” Alikuwa na haki kufanya hivyo, inaonekana. Bali yeye hakuwa na haki kufanya hivyo.

¹⁸⁴ Kama nilivyosema jana usiku, huna wazo lolote. Ni wazo Lake, unaona, kile Yeye afanyacho. “Mapenzi Yako yafanyike, omba hivi.” Yeye si tarishi. Yeye ni Mungu. Angalia, “Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike.”

¹⁸⁵ Ndipo wakati alipomfikia Yeye, alimwendea kwa njia sahihi. Alisema, akampa sifa Yake sahihi, “Bwana!” Sio kumkemea, bali, “Bwana, kama Wewe ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa.” Loo, jamani! Ninaweza kumwona Yeye akivuta pamoja maskini mwili Wake, uliochoka. Na—na Yeye akasema... “Kama Wewe ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote Wewe utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa Wewe.” Unaona, alijua kile Mungu wa uumbaji alikuwa. Alijua Yeye alikuwa ni Masihi mpakwa mafuta. Alimwendea vizuri, juu ya magoti yake, kasema, “Bwana, kama Wewe ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote Wewe utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa Wewe.” Loo, laiti tungaliweza tu kuwazia hilo! “Hata sasa, Bwana, lolote Wewe utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa Wewe.”

¹⁸⁶ Akasema, “Mimi ndimi ufufuo na Uzima.” Hakuna mtu yeyote mwingine angaliweza kusema hilo. “Mimi ndimi ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Yeyote aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Je! unasadiki haya?”

¹⁸⁷ Akasema, “Naam, Bwana. Ninaamini kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu aliyepaswa kuja ulimwenguni.”

Akasema, “Mmemzika wapi?”

¹⁸⁸ Nilikuwa nikizungumza na mwanamke fulani si muda mrefu uliopita, naye akaniambia, akasema, “ni—ni—ninapenda kukusikia ukihubiri, Ndugu Branham, ila,” kasema, “kuna kasoro moja tu uliyo nayo.”

Nikasema, “Asante,” kasoro moja tu. Nikasema, “Ni nini hiyo?”

Akasema, “Unajivunia kupita kiasi juu ya Yesu, kuwa ni Mungu.”

Nikasema, “Ninatumaini hiyo ndiyo ya pekee Yeye anayoweza kupata kwangu,” nikasema.

¹⁸⁹ “Unajivunia sana kuhusu Yesu kuwa ni Mungu.” Kasema, “Yeye hakuwa Mungu.”

Nikasema, “Loo, naam, Yeye alikuwa Mungu.”

Akasema, “Vema, unamfanya kuwa Mungu.”

¹⁹⁰ Nikasema, “Yeye ama alikuwa ni Mungu au mdanganyifu mkubwa kuliko wote ulimwengu ulipata kuwa naye.” Unaona? Tena nikasema, “Alikuwa Mungu.”

Akasema, “Yeye alikuwa Mwanadamu tu. Asingeweza kuwa ni Mungu.”

Nikasema, “Alikuwa. Alikuwa Mungu na mwanadamu, pamoja.”

Ndipo akasema, “Ulisema unaamini Biblia.”

Nikasema, “Naam, mama, ninaamini.”

¹⁹¹ Ndipo akasema, “Kama nikikuthibitishia, kwa Biblia yako mwenyewe, kwamba Yeye hakuwa Mungu, utakubali?”

¹⁹² Nikasema, “Hakika, kama Biblia ilisema Yeye hakuwa. Bali,” nikasema, “Siamini liko katika Biblia.”

¹⁹³ Akasema, “Katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 11, Biblia ilisema, ‘Wakati Yesu aliposhuka kwenda kwenye kaburi la Lazaro,’ Biblia ilisema, ‘Yeye alilia.’” Tena kasema, “Kama Yeye alilia, asingeweza kuwa ni Mungu, na analia.”

¹⁹⁴ Nikasema, “Vema, mama, hilo halistahimili.” Nikasema, “Ninataka kukuambia.” Nikasema, “Hilo ni jembamba kuliko mchuzi uliotengenezwa kutokana na kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa,” nikasema, “kwa sababu hilo halitasimama kwa Biblia.” Nikasema, “Tazama, Yeye anateremka kwenye kaburi, unaona, na Yeye alisimama mbele ya kaburi, ndipo Yeye akasema, akanyosha maskini mwili Wake na kusema, ‘Lazaro, njoo huku!’”

¹⁹⁵ Huenda alikuwa ni Mwanadamu, akilia; bali wakati Yeye alipomwita mtu huyo kutoka kaburini, aliyekuwa amekufa kwa siku nne, na nafsi yake ilikuwa imeenda safari ya siku nne mahali fulani! Sijui mahali ilipokuwa, wala hata wewe. Kwa hiyo, hata hivyo, Yeye alimwita akarudi. Uharibifu ulimjua Bwana wake. Nafsi ilijua Muumba wake. Na mtu, aliyekuwa amekufa, alisimama kwa miguu yake na kuishi tena, baada ya kufa siku nne. Huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa ni Mungu!

¹⁹⁶ Ilikuwa ni Mwanadamu wakati Yeye aliposhuka kutoka mlimani, usiku ule, na alikuwa na njaa, akatazama kote kwenye mti wa mkuyu, kupata kitu cha kula. Alikuwa ni Mwanadamu wakati Yeye alipokuwa na njaa. Lakini wakati Yeye alipochukua biskuti tano na samaki wawili, na kulisha watu elfu tano, huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu.

¹⁹⁷ Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati alipokuwa analala huko nyuma ya chombo, usiku ule, ambapo pepo elfu kumi wa baharini waliapa wangemzamisha Yeye. Na maskini chombo hicho katika hayo mawimbi, kama kifuniko cha chupa huko nje mahali fulani, kikielea huku na huko namna hiyo. Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati Yeye alipokuwa amelala, Yeye alikuwa amechoka, nguvu zilikuwa zimemtoka. Bali wakati Yeye alipoweka mguu Wake demani mwa chombo, na kutazama juu na kusema, “Amani, tulia,” na pepo na mawimbi yakamtii, huyo

alikuwa zaidi ya mwanadamu. Huyu alikuwa ni Mungu ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake!

¹⁹⁸ Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati Yeye alipokufa msalabani, akililia rehema. Hiyo ni kweli. Lakini Yeye alikuwa Mungu kwenye asubuhi ya Pasaka, wakati Yeye alipovunja muhuri, uliokuwa kaburini, akafufuka na kupaa Juu, (naam, bwana) anaishi milele kufanya maombezi. Kila mume na mke, aliyewahi kuwa na maana yoyote, aliamini hilo. Naam, bwana.

¹⁹⁹ Ni yeye yule jana, leo, na hata milele! "Je! unasadiki haya?" [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naam, bwana. Yeye ni mkuu tu papa hapa miongoni mwetu, usiku wa leo, kama Yeye alivyokuwa wakati ule. Unasadiki haya? ["Amina."] Yeye ni Mponyaji yule yule, usiku wa leo, Yeye alivyokuwa wakati ule. Je! unasadiki haya? ["Amina."] Hakika. Hawezi kushindwa. Shikilia. Shikilia nafasi yako katika Kristo, maungamo yako. Shika sana maungamo yako katika Kristo.

²⁰⁰ Alishikilia ndipo akapata ufufuo wa kaka yake.

²⁰¹ Mwanamke Mshunami alishikilia mbele za Eliya. Eliya alipitia na kumbariki, na kumwambia kwamba atakuwa na mwana. Mwana huyo alifikia yapata umri wa miaka kumi na miwili. Akiwa nje kondeni, hapana shaka alipatwa na ugonjwa uletwao na kuchomwa na jua. Mwanamke huyu alikuwa amemfadhili sana Eliya. Alikuwa ni mwanamke Mshunami, na alitoka katika nchi ya Shunami. Na aligundua... Alimwambia mume wake, akiwa ni mtu tajiri, akasema, "Naona kuwa mtu huyu ambaye hupita hapa ni mtu mtakatifu." Akasema, "Hebu tumpe fadhili." Kasema, "Hebu tumjengee chumba kidogo ubavuni mwetu mwa nyumba hapa, akija, na kumwekea kitanda kidogo na jagi ndogo hapo nje, ili aweze kupumzika."

Naye mume wake akasema, "Hilo litakuwa jema sana."

²⁰² "Kwa hiyo ukiwafanyia jambo hawa wadogo, unanifanyia Mimi," Yesu alisema.

²⁰³ Kwa hiyo akasema, akamwambia mtumishi wake, Gehazi. Kasema, "Nenda kamwulize, je! ninaweza kuongea na jemadari, ama ninaweza kumfanyia nini?"

Akasema, "La, ninaishi miongoni mwa watu wangu. Niko sawa."

Ndipo Gehazi, Gehazi akasema, "Lakini hana watoto wowote."

²⁰⁴ Kasema, "Nenda ukamwambie." Kukaja ono. Kasema, "Nenda ukamwambie, yapata wakati huu yeye anaenda kujifungua mtoto." Naye alijifungua.

²⁰⁵ Mvulana huyo akafikisha yapata umri wa miaka kumi na miwili. Yake, baba yake akiwa ni mkongwe. Alikuwa nje kondeni, siku moja, hapana shaka alipata ugonjwa utokanao na kuchomwa na jua. Ilikuwa yapata adhuhuri, akaanza

kulia, “Kichwa changu! Kichwa changu!” Akamrudisha ndani mvulana. Na yeye akalala pajani mwa mama yake mpaka akafa. Angalia ni mahali panapostahili jinsi gani, yeye alimpeleka huko katika chumba kile ambapo nabii alikuwa amelala katika kitanda kile. Unaona?

²⁰⁶ Ndipo akamwambia mtumishi, “Mtandike nyumbu, na uanze mwendo kuelekea Mlima Karmeli. Huko juu kuna pango mahali fulani, ambapo mhubiri huyu anaishi. Yeye alikuwa ndiye aliyekuwa na uwezo kuona ono, akasema kuwa nitajifungua huyu mwana; na kama yuko karibu na Mungu vya kutosha, yeye ni mjumbe wa Mungu wa majira haya. Na mimi ninajua, kama angeweza kuniambia ni kwa nini, kama ningemfikia, angeweza kuniambia sababu ya Mungu kumchukua mtoto huyo. Hebu nipande huko juu.” Akasema, “Ikiwa yeyote atakusalimu, usimsalimie. Wala usisimame; zidi tu kuenda.”

²⁰⁷ Loo, ninapenda hilo! Wakati wa dharura sasa. Watu wanakufa, hatupaswi kuwa tukicheza huku kwenye barabara. Zidi kusonga. Na yeye alishikilia.

²⁰⁸ Na Eliya. Unajua, Mungu hawaambii manabii wake kila mara kila kitu kinachoenda kutukia. Alitazama juu na akamwona akija, akasema, “Huyu hapa Mshunami anakuja.” Tena kasema, “Amejaa huzuni, lakini Mungu amenificha hilo.” Akasema, “Kimbia, umlaki.” Ndipo yeye. . .

²⁰⁹ Akasema, “Je! hujambo? Mume wako hajambo? Mwana wako hajambo?”

²¹⁰ Ninapenda hili, huko kushikilia mpaka alipoingia katika uwepo wa mjumbe. Na yeye akasema, “Hatujambo.” Mum-. . . mume wake akiminya mikono yake, na kutembea huku na huku chumbani, akilia, naye mtoto amelazwa kitandani, amekufa, lakini, “Hatujambo.” Amina. Kwa nini? alikuwa amefikia lengo lake. Alikuwa ametimiza lengo lake. Kushikilia kwake, kwamba angeweza kumfikia mtu wa Mungu, mtu wa Mungu angeweza kumwambia ni kwa nini. Ndipo akamwangukia mguuni pake na kufichua kilichokuwa kimetendeka.

²¹¹ Sasa aliinama na kuchukua fimbo yake, na kumwambia mtumishi wake, “Itwae hii, na uende ukaiweke juu ya huyo mtoto.” Sasa, nafikiri hapo ndipo Paulo alipopata kuweka lesa juu ya watu. Unaona, kwa sababu Eliya alijua kwamba kila kitu alichokigusa kilibarikiwa, bali laiti angaliweza kumfanya mwanamke huyo kuamini hilo!

²¹² Lakini imani ya mwanamke huyo haikuwa katika hiyo fimbo, ilikuwa katika nabii. Unaona? Ndipo mwanamke huyo akasema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, na nafsi yako haifi,” unaona, alikuwa ameshuhudia pale alikuwa na Uzima wa Milele. Kasema, “Na nafsi yako haifi, sitakuacha.” Loo, jamani, dumu nalo! Jambo ndilo hilo.

²¹³ Hiyo ndiyo njia ya kupata kile unachotaka. Kama huyu mwanamke Mshunami, kama huyu mwanamke Msirofoinike, dumu nalo! Dumu papo hapo. Dumu moja kwa moja na Kristo. Lishike, usiku wa leo, na ushikilie hapo. Kamwe usisonge. Kesho, kama mtu fulani akisema, “Hiyo ni ninii tu. . .” Wazibie tu masikio yao. Wewe una imani: Wewe dumu hapo.

Kasema, “Sitakuacha.”

²¹⁴ Naye Eliya akasema, “Vema, siwezi kumwondosha, afadhali niandamane na yeye.” Kwa hiyo akafunga viuno vyake, na huyo akaenda.

²¹⁵ Angalia wakati alipoingia chumbani. Hakujua la kufanya. Kamwe hakuomba. Alitembea tu huku na huku, juu-chini sakafuni, mpaka akahisi Roho wa Mungu akija juu yake. Ndipo akaenda akajilaza mwenyewe juu ya mtoto huyo, naye akapiga chafya mara saba, na akafufuka.

²¹⁶ Martha alijua, kama Mungu alikuwa ndani ya huyo nabii, hakika Yeye alikuwa ndani ya Mwana Wake, unaona, na hiyo ndiyo sababu aliweza kushikilia.

²¹⁷ Na iwapo tumekuwa na maelfu ya miaka ya ujuzi tangu wakati huo, kujua kwamba Mungu hutimiza ahadi Yake, jinsi tunavyopaswa kushikilia usiku wa leo wakati tunapoweza kuona Uwepo wa Yesu Kristo, loo, jamani, na kuangaza kama nyota!

²¹⁸ Ninakumbuka usiku mmoja, nyumbani si muda mrefu uliopita, kulikuwa na mwanamke, na mimi sikujua mwanamke huyo alitaka kuombewa. Sikuenda chini na kuwaombea wagonjwa usiku huo. Na mahali hapo palikuwa pamejaa sana! Na baadhi ya wadhamini wangu walioketi hapa ndani mahali fulani, usiku wa leo, walikuwapo. Na kulikuwa na mwanamke aliyekuja kutoka California, alikuwa na uvimbe wenye uzito wa ratili hamsini. Asingeweza kuenda kwa daktari; ndipo basi, walipomfanya kwenda, ulikuwa mkubwa kupita kiasi cha kupasuliwa, uvimbe mkubwa wa maji. Na yeye alikuwa nje kabisa namna *hii*, uvimbe mkubwa mzito. Nao walikuwa wamemleta hapo. Walikuwa wamemleta. Wasingeweza kumleta kwa motokaa. Iliwabidi kumweka katika trela, kitu kama hicho, ili kumleta. Nao walikuwa wamemleta ndani. Sikujua, na mimi nikaendelea tu na kunena. Ndipo yeye akasema, “Vema, hivi haendi. . .” Nilifanya wito wa madhabahuni. Kasema, “Hivi haendi kuwaombea wagonjwa?”

Kasema, “La.”

²¹⁹ Akasema, “Ni mlango upi anaotokea?” A-ha. Sasa wazia tu, imani yake! Ndipo wakazunguka na huyo mwanamke, na kumbeba kuzunguka kwenye mlango wa nyuma, mahali ambapo ninapitia kuingia chumba cha mchungaji cha kusomea na kuenda kwenye motokaa yangu.

220 Naye mwanamke huyo akiwa amelala pale, alinishika kwa mguu wa suruali, ndipo akasema, “Ndugu Branham!” Safi, loo, jamani, alikuwa nje namna *hiyo*. Kasema, “Kama utaweka tu mikono yako juu yangu, Mungu atanifanya mzima.” Nami nikafanya hivyo.

221 Ndipo yapata miezi mitatu kuanzia hapo, nilikuwa kwenye mkutano. Na hapa alisimama, akiwa tu mzima kama mwanamke yeyote nchini; na nilimwalika dada yeyote hapo aende na yeye ndani ya chumba, na avue nguo na aone kama amefanyiwa upasuaji au sivyo.

222 Kwa nini? Alishikilia. Aliyakinia kupata kile kilichomleta. Hivyo ndivyo ilivyo. Naam, bwana. Imani yao ilikuwa imelishika Neno.

223 Mikaya, wakati mmoja, wakati alipoitwa ndani. Wakati Yehoshafati alipofanya ushirikiano na Ahabu, hapo ni pale mwaminio na asiyeamini wanachanganyikana. Na yeye alisema walikuwa wanataka kuenda kupiga vita; walikuwa wanapanda kwenda mahali, kuchukua nchi yao wenyewe. Kimsingi, ilikuwa ni yao. Kasema, “Ni kwa nini Waashuri hawa wawe wakila mahindi ambayo ni ya Israeli? Yohua alitupatia hiyo!” Hiyo ni kweli kabisa. Kwa hiyo walienda na walikuwa na shule kubwa ya wahubiri huko chini, seminari nzima; tano, mia nne au tano ya hao, wanaume wa Kiebrania waliofunzwa vizuri.

224 Na kwa hiyo Yehoshafati akasema, akiwa ni mtu mwenye haki, alisema, “Lakini hivi si tungemtaka Bwana shauri?”

225 Akasema, “Loo, naam, labda hiyo ni kweli.” Ahabu, unajua alikuwa ni jamaa wa namna gani, kwa hiyo anateremka. Kisha kasema, “Ninalo jawabu, nina manabii mia nne. Tutawaleta hapa juu.”

226 Kwa hiyo wakateremka kule chini, na mmoja wao, Zedekia, ninaamini alikuwa, alijitengenezea pembe mbili kubwa na kupanda huko juu, akisema, “BWANA ASEMA HIVI. Kwea, ni mali yako. BWANA ASEMA HIVI, utawasukuma hao Waashuri moja kwa moja mpaka nje ya nchi, kwa pembe hizi.”

227 Yehoshafati akaangalia huku na huku, mwajua, ndipo a— akasema, “Hivi hakuna mwingine mmoja?”

228 “Mwingine? Wakati manabii mia nne wa Kiebrania waliofunzwa kutoka shuleni, unataka nini na mwingine mmoja? Tunao mia nne! Seminari yote ipo hapa, na wote kwa nia moja, wakisema, ‘Kwea, Bwana yuko pamoja nawe. BWANA ASEMA HIVI.’”

Yehoshafati akasema, “Vema, hivi huna mwingine mmoja?”

229 Akasema, “Loo, nina mmoja zaidi niwezaye kumtaka shauri,” kasema, “huyo ni Mikaya mwana wa Imla, ila,” kasema, “Ninamchukia.” Loo, hakika. Naam. Kasema, “Vema, hata

hakubaliani na haya madhehebu na kadhalika.” Kasema, “Sisi—sisi, vema, inakubidi. Hapo, kuna jamaa wa ajabu,” wakasema.

“Loo,” akasema, “mfalme asiseme hivyo. Nenda kamlete.”

²³⁰ Kwa hiyo wakamtuma mmoja wa jamaa hao huko chini, kasema, “Sasa, Mikaya, unajua umetolewa nje ya shirika, huna ushirika na wao tena. Lakini sasa ikiwa tu utasema, jambo lile lile wanalofanya, huenda wakakurudishia kadi yako ya ushirika, ukirudi tena.” Je! ungeweza kuwazia kuzungumza na nabii kwa njia hiyo?

²³¹ Mikaya akasema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, nitasema tu kile Yeye asemacho.” Sasa wewe hapo. Amina. Jambo ndilo hilo.

“Vema, unajua kile wangeweza kukufanyia?”

²³² “Hicho hakijalishi. Nitasema tu kile Yeye asemacho.” Akarudi kwake, akasema, “Sasa hebu niwe na usiku wa leo, na mimi nitaona kile Bwana alichosema.”

²³³ Akarudi asubuhi iliyofuata, ndipo akasema, “Kwea. Naam, bwana. Kwea. Bali niliona Israeli, kama kondoo waliotawanyika, bila mchungaji.”

²³⁴ Basi huyu Zedekia anakuja, na anachukua mkono wake na kumpiga kofi moja kwa moja mdomoni, “maskini huyo mtakatifu anayejibingirisha,” akaketi chini na kusema, “Roho wa Mungu alienda wapi wakati alipotoka kwangu?”

Akasema, “Utaona.”

Kwa hiyo akasema, “Nini kuhusu hilo?”

²³⁵ Kasema, “Niliona ono jana usiku. Nilimwona Mungu ameketi mahali palipoinuliwa, na katika Hili, Enzi Yake kubwa iliyoinuliwa.” Tena kasema, “Yeye, wote walikuwa wamemzunguka. Walikuwa na baraza, ‘Ni nani tunayeweza kumtuma aende chini kumdanganya Ahabu, kumfanya apande huko juu kutimiza kile alichosema nabii Eliya? Ninaweza kufanya nini kuhusu hili?’” Ndipo kasema, “Pepo wa uwongo akasimama, na kusema, ‘Nitaenda huko chini na kuingia ndani ya hao manabii, na kuwafanya kusema uongo.’ Ndipo Bwana akasema, ‘Wewe ndiwe uwezaye kufanya hilo, maana walifunzwa kiseminari, mwajua.’ Kasema, ‘Wewe nenda kafanye hivyo. Hayo ndiyo yote uwezayo kufanya.’” Akaenda huko chini, na akafanya hivyo!

²³⁶ Sasa unasema, “Vema, ni nani angeweza kujua kilichokuwa sahihi?” Mikaya alikuwa pamoja na Neno!

²³⁷ Unawezaje kubariki kile ambacho Mungu amelaani? Unawezaje kuwaambia watu kwamba wanaweza kuishi namna hii na kufanya mambo haya, na hata hivyo wadumishe ushirika wa Yesu Kristo? Huwezi kufanya hivyo. Lazima uzaliwe tena na kujazwa na Roho Mtakatifu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

“... Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi ni kwa ajili ya watoto wenu, na wale walio mbali, wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu.” Hilo lilikuwa ndilo agizo. Hutaki kuharibu agizo hilo.

²³⁸ Daktari anaweza kukuandikia fomula fulani. Na wewe unapeleka hilo kwa tabibu bingwatapeli, na yeye asiichanganye ipasavyo, utamwua mgonjwa wako.

²³⁹ Na hiyo ndiyo shida leo hii, mmeingiza kupeana mikono na kila kitu kingine, badala ya Hilo. Rudini! Mungu alimruhusu Petro kuandika agizo la Milele kwa ajili ya wokovu. Halijawahi kubadilishwa, wala Hilo haliwezi kubadilishwa. Kupeana mikono na kujiunga na kanisa, na kadhalika, havitachukua mahali pa Hilo. Halina budi kurudi, Neno kwa Neno, jinsi Hilo lilivyoandikwa Hapo. Hilo ndilo agizo walilotumia kote katika Biblia. Walilitumia mpaka Baraza la Nikea, ndipo basi wakabadilisha agizo hilo. Hiyo ndiyo sababu tunao washiriki wengi waliokufa leo hii. Kweli. Inakubidi kupata agizo halisi. Halafu ujue, kama lilifaulu kule, litafaulu sasa, “Ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na wale walio mbali, wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu.” Usiingize chochote kwenye Hilo. Usiongeze chochote Kwake. Ukiongezea chochote kwa Hilo...

²⁴⁰ Kumbukeni, agizo ni dawa tu ya kutosha humo ndani kuondoa ugonjwa, na ya kutosha kuua ya kutosha ya dawa kwa ajili ya mgonjwa. Na usiponinii, ukiweka dawa nyingi kupita kiasi ndani yake, ama kitu kingine ambacho hakitafanya kazi, ukipunguza nguvu zake kupita kiasi, halitasaidia mgonjwa. Ukiweka sumu nyingi kupita kiasi ndani yake, litamwua mgonjwa. Inabidi liwe tu sahihi.

²⁴¹ Na Yeye aliandika agizo la Milele, kwa kuwa ni kwa ajili ya kila kizazi. Si kupeana mikono, kujiunga na kanisa, na mambo haya yote mengine. Alisema, “Tubuni, ndipo basi mbatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, na nyinyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Imeahidiwa kwenu na kwa watoto wenu.”

²⁴² Walichukua hilo agizo na kulitekeleza kwenye kaunta kubwa ya Mungu. Basi wakati walipofanya hivyo, kwenye Siku ya Pentekoste, waliwaponya wagonjwa, walifanya kila kitu kilichokuwepo kufanywa; maana ilikuwa ni Mungu, Kristo ndani yao. Vema.

²⁴³ Mikaya alijua kwamba hilo lilikuwa ni Neno la Bwana, kwa sababu lilikuwa hasa kile Bi—Biblia, Nabii halisi, alichosema. Mungu alikuwa amemlaani mtu huyo na kumlaani mke wake, kwa sababu ya uovu wao. Na ikiwa (wao) Yeye alikuwa amekilaani, watu hawa wangeweza kuzunguka na kukibariki?

²⁴⁴ Hapa ndipo mahali walipotoa wazo lao. Nchi hiyo ni yao. Kwa kweli walipewa hiyo. Lakini dhambi zao zilikuwa zimewaondoa kwake. Kwa hiyo waliwaza, kwa sababu nchi ilikuwa ni yao, kwamba hiyo ndiyo yote iliyowapasa kuwa nayo. La, bwana.

²⁴⁵ Ni kwa masharti. Kikamilifu. Unaweza kuwa na uponyaji wa Kiungu, unaweza kuwa na wokovu, unaweza kuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, bali hayo ni juu ya masharti, kwamba umetimiza masharti ya Mungu. Nje ya hayo, si kwa ajili ya mtu yeyote ila waaminio.

²⁴⁶ Mtu aliniambia, si muda mrefu uliopita, mhudumu, alisema, "Sijali kama ungeinuka na kuwa na taarifa za madaktari za kufufua wafu, na kila kitu kingine," kasema, "Siamini hiyo."

Nikasema, "Hakika siyo, si kwa ajili ya wasioamini."

²⁴⁷ Ni kwa waaminio pekee. Halikutolewa kwa ajili ya wasioamini. Limetumwa kwa waaminio pekee. Ni kwa ajili ya hao pekee, ni kwa ajili ya waaminio, sio wasioamini. Hakika, wanakubali hapo—hapo kilicho kasoro.

²⁴⁸ Lakini Mikaya alijua. Wakati alipoona ono lake lilikuwa hasa na Neno la Mungu, basi alijua lilikuwa sahihi. Na yeye alishikilia, kama ilichukua maisha yake au siyo. Akasema, "Utagundua, wakati haya yote yakitendeka ambayo nimesema, yanapokuja kutimia, ndipo utajua mahali Hilo lilipo."

²⁴⁹ Njia ile ile, mtu kipofu, asingeweza kubishania theolojia yao; lakini alijua macho yake yalifunguka, kwa hiyo alishikilia sana kuhusu hilo. Kama vile Filipo, na kama vile Nathanaeli, yule mwanamke kisimani, wote walishikilia baada ya kumshika Mungu.

²⁵⁰ Sasa katika kufunga, tunaenda kuanzisha mstari wa maombi sasa hivi katika dakika moja, jambo fulani tu linanijia niani sasa hivi tu kusema.

²⁵¹ Si muda mrefu uliopita, nilikuwa Meksiko, huko chini. Bwana alikuwa amenituma huko chini kwenye mji wa Meksiko, ule mduara mkubwa pale. Loo, watu walikuwa maelfu mara maelfu. Na usiku uliotangulia, kulikuwa na mzee kipofu aliyekuja jukwaani, ndipo, sasa, lilikuwa moja ya matamasha mabaya kuliko yote. Kulikuwa na . . .

²⁵² Ni wangapi wanamjua Ndugu Espinoza? Unaona, wapo wengi. Hakika. Vema, sasa, yeye alikuwa ni mkalimani wangu. Anaweza kuwaambia hili. Na kulikuwa na mtu kipofu aliyepanda juu kwenye jukwaa, maskini mzee Mmeksiko.

²⁵³ Na uchumi wao ni mbaya sana huko. Kwa mfano, labda mwa—mwashu atapata peso kadhaa kwa siku, labda tuseme peso tano kwa siku. Sijui kile ingefanya. Na huyo ni Pedro, na anapata . . . Yeye ni mwashi, kwa hiyo yeye hupata peso tano kwa siku, lakini inambidi kufanya kazi siku tano kujinunulia

jozi ya viatu, unaona, katika uchumi wao. Na vipi kuhusu maskini Pancho basi, Chico, maskini yule ambaye inabidi afanye kazi hapa nje na anapata peso mbili tu kwa siku, na anao watoto watano wa kulisha? Lakini inawabidi kuweka ya kutosha kutokana na hizo, kuwasha kandili ya mafuta juu ya madhabahu ya dola milioni moja, kwa ajili ya dhambi zake, unaona. Hicho ndicho kilichoniunguza, na kwa hiyo kuwaona wakifanya vitubio kwa wanawake waliokufa, na kutambaa kwa magoti yao, na mambo kama hayo.

²⁵⁴ Kwa hiyo, usiku mmoja, mzee huyu akaja kupitia jukwaani, hakuwa na viatu mguuni. Nywele zake zilikuwa na mvi. Alikuwa na kofia chakavu iliyofungwa na kamba. Alikuwa anakuja kupitia jukwaani. Nikamwangalia maskini jamaa huyo. Na hapa nilikuwa nimesimama nimevaa jozi nzuri ya viatu na suti nzuri. Alikuwa kipofu. Alikuwa anatembea namna *hii*. Ndipo yeye akasema, na akaendelea kusema jambo fulani. Bila shaka, siwezi kuzungumza maneno machache tu ya Kihispaniola. Akavuka akaja upande *huu*. Ndipo nikamfikia, nikaweka... nilifikiri hakuna mtu angaliniona; Ni—niliweka mguu wangu nje namna *hii*, kuona ikiwa mguu wangu, kama kiatu changu kingemtosha. Kama kingemtosha, nilikuwa ninaenda kuvivua na kumfanya avivae. Na, halafu, mguu wake ulikuwa mkubwa zaidi. Na kwa hiyo kwa namna fulani ni—ni... Nikasema, “Ubarikiwe, baba.”

²⁵⁵ Na nikainua mabega yangu, kuona ikiwa koti langu lingemtosha. Na lisingemtosha, na kubwa zaidi. Hakuwa na shati, amevaa tu koti kuukuu. Na mimi nikawazia, “Maskini jamaa mkongwe, labda hajawahi kuwa na chakula kizuri maishani mwake.” Suruali yake kuukuu, iliyochanika, na vumbi kila mahali juu yake. Na hapa ibilisi hata alikuwa amempofusha. Na hapo alikuwa, akitembea kupita pale, akisema jambo fulani. Nami nikawazia, “Kama baba yangu angaliishi, angekuwa yapata umri wa mzee huyo.” Nikawaza, “Ee Mungu!”

²⁵⁶ Ndipo nikamkumbatia. Lazima uwahurumie watu. Usipowahurumia, hakuna haja ya kuomba, huna huruma. Ndipo nikamkumbatia.

²⁵⁷ Nikasema, “Usiseme hili, Ndugu Espinoza.” Hawatafsiri maombi, hata hivyo.

²⁵⁸ Kwa hiyo nikasema, “Baba wa Mbinguni, mrehemu.” Niliweka mikono yangu juu yake namna hiyo.

²⁵⁹ Akapaza sauti, “Gloria de Dios!” Hilo linamaanisha, “Utukufu kwa Mungu.” Unaona? Alitazama kote namna *hiyo*, na mzee huyo aliweza kuona vizuri tu kama nilivyoweza kuona. Hapo akaenda, akitembea kutoka jukwaani.

²⁶⁰ Vema, u—usiku uliofuata, walikuwa na yapata, loo, karibu kutoka hapa hadi mlangoni, lingekuwa ndilo jukwaa, na mashali tu makuukuu na maskini nguo zilizochanika zimelundikwa pale juu, kuombewa. Na kulikuwa kunamwagika mvua, wasingeweza

kupata . . . Na wao walikuja hapo asubuhi hiyo, yapata saa mbili au saa tatu; na mimi nisingeweza kuwa hapo mpaka usiku huo, yapata saa mbili au tatu. Kwa hiyo kulikuwa na watu wengi sana hapo. Hakuna viti vya kukalia, kama mlivyo navyo. Waliegemeana mmoja na mwenzake. Wakisimama hapo kwenye mvua hiyo, wanawake wakiwa na nywele zao zote zimening'inia chini, zimeloa, wakingojea tu kusikia Neno la Uzima.

²⁶¹ Na Jenerali Valdivia aliniingiza ndani. Nadhani mlimjua, yeye ni mmoja wa wafanyabiashara Wakristo. Na mprotestanti wa kwanza kuwahi kuwekwa chini ya ulinzi wa serikali. Jenerali Valdivia huko Meksiko, kwa hiyo wakati huo nilikuwa . . .

²⁶² Usiku huo niliingia ndani, walinishusha kwa kamba fulani, nyuma kurudi nyuma ya uwanja. Niliingia ndani yake namna hii, kwa kamba, kutoka nyuma ya motokaa. Na wakati nilipofika chini ndani ya uwanja, nilitembea pale. Ndipo Billy akanijia, mwana wangu, akasema, “Kuna jamaa pale amekuwa akisambaza kadi za maombi.” Ninamwita *Manana*, hilo linamaanisha “kesho,” alikuwa mwenda pole sana, na yeye asingeweza kuja kunipata. Kwa hiyo angesambaza kadi za maombi.

²⁶³ Ndipo Billy akasema, “Vema,” akasema, “Baba, yuko mwanamke huko chini aliye na mtoto aliyekufa.” Na nyinyi nyote mliona makala haya katika *Sauti* ya Wafanyabiashara. Na akasema, “Ana mtoto aliyekufa.” Tena kasema, “Hatuna kadi zozote za maombi.” Pia akasema, “Nina karibu mabawabu mia tatu ambao hawawezi kumshika.”

²⁶⁴ Na yeye—yeye alikuwa ni maskini mwanamke mdogo, msichana tu, msichana mrembo sana. Na yeye alikuwa . . . alikuwa na maskini mtoto huyu aliyekufa, na blanketi ndogo ya samawati yenye milia juu yake, akishikilia maskini mwili uliokauka, yapata urefu huu, mikononi mwake, alikuwa amesimama hapo tangu asubuhi hiyo. Mtoto huyo alikufa saa tatu, na hii ilikuwa yapata saa nne usiku huo. Na kwa hiyo alikuwa amebeba maskini mtoto huyu mikononi mwake.

²⁶⁵ Na mimi nikasema—nikasema, nikasema, “Vema, waambie tu hao mabawabu kumzuilia mbali. Ukimweka ndani pamoja na watu hao wanaobeba kadi ya maombi,” nikasema, “itafanya . . .” Ndipo nikasema, “Hivi hutamwambia aje karibu?”

²⁶⁶ Kasema, “Huwezi kumwambia chochote.” Kasema, “Yeye kamwe hatakisikiliza.”

Na mimi nikasema, “Vema, mabawabu wa kutosha pale, hakika, kumzuilia mbali.”

Kasema, “Huwezi kufanya hivyo.”

²⁶⁷ Nikasema, “Ndugu Moore.” Ni wangapi wanaomjua Ndugu Jack Moore? Yeye ni . . . Nikasema, “Asingeweza kujua tofauti

kati yangu na wewe. Hanijui.” Nikasema, “Wewe nenda huko chini na umwombee, Ndugu Moore.”

Akasema, akasema, “Sawa.”

²⁶⁸ Nikasema, “Wewe nenda huko chini na umwombee mtoto huyo. Na hilo litamridhisha, na yeye ataenda nyumbani.”

Akasema, “Sawa.”

²⁶⁹ Kwa hiyo nikageuka kurudi nyuma. Nilikuwa nikizungumzia “imani kuwa ni hakika ya mambo yatarajiwayo,” na kuhusu Yesu, na jinsi Yeye alivyofanya wakati Yeye alikuwa hapa duniani, akiwazungumzia. Na punde tu nilipoanza kunena, nilitazama mbele zangu, katika ono, na kulikuwa na maskini mtoto mwenye uso mweusi, na alikuwa—alikuwa akicheka na mimi. Ndipo nikatazama tena.

Ndugu Espinoza akasema, “Ni nini, Ndugu Branham?”

²⁷⁰ Nikasema, “Usijali, Ndugu Espinoza. Uweke tu umati katika hali ya makaribisho, dakika moja tu.”

²⁷¹ Ndipo nikaondoka. Nikasema, “Ngoja kidogo, Ndugu Moore.” Na kwa hiyo alikuwa amefika chini mahali maskini... mahali maskini mwanamke huyo alipokuwa. Ndipo nikasema, “Mwambie amlete mtoto huyo hapa.”

²⁷² Basi kwa hiyo hapa akaja juu jukwaani. Aliinamisha goti moja, akiwa na rosari mkononi mwake. Alikuwa anasema, “padri,” hilo linamaanisha “baba,” mnajua.

²⁷³ Nikasema, “Simama sasa. Simama.” Nikamfanya kusimama. Nikasema, “Mtoto amekufa?” Asingeweza kuelewa. Machozi yakitiririkia maskini uso wake, na nywele zake zikisambaa chini. Sasa hii ni kweli; hiyo hapo Biblia yangu. Na, unaona, niliweka mkono wangu juu ya maskini mtoto huyo, na nilifikiri kwamba hilo lingemridhisha. Sikujua huyo alikuwa ndiye mtoto yule mchanga. Nisingeweza kusema hilo.

²⁷⁴ Ndipo nikasema, “Baba wa Mbinguni,” nikasema, “mbele zangu kulikuwa na ono la mtoto mchanga, na labda huyu ndiye. Na kama ndivyo ilivyo, ninakuomba Wewe, Bwana, kuiheshimu imani ya maskini mwanamke huyu, kumrudishia mtoto wake mchanga.”

²⁷⁵ Na wakati huo tu jamaa huyo mdogo alipiga mayowe na kuanza kulia, kwa nguvu tu alivyoweza. Naye maskini mwanamke huyo, hakujua la kufanya. Kwa hiyo yeye... Nikamwambia Ndugu Espinoza. Nikasema, “Sasa usiliseme. Basi ngojea, wewe nenda na uache daktari atie sahihi taarifa kwa hilo.

²⁷⁶ Na katika *Sauti*, Sauti ya Wafanyabiashara Wakristo, hivi majuzi tu, ilitokea. Unaona, kabla hujaandika chochote, inakubidi kuwa na ushahidi kwamba hicho ni kweli. Daktari alitia sahihi taarifa, “Mtoto huyo alikufa, akiwa na nimonia;

upumuaji wote ulimwondokea, asubuhi hiyo kwenye saa tatu,” ofisini mwake. Na hii ilikuwa ni saa nne na kitu usiku huo, wakati alipofufuka tena, kwa sababu maskini mwanamke alishikilia.

²⁷⁷ Kama Mungu aliweza kufungua macho ya mtu aliye kipofu, Yeye pia aliweza kumrudisha mtoto wake mchanga. Yeye angali ni Mungu yule yule, usiku wa leo, ewe rafiki. Lazima ushikilie, kutimiza chochote. Vipi kama yeye angalisikiliza, na kusema, “Vema, mtoto huyo mchanga amekufa,” na kuachilia tu na kuendelea? Unaona? Basi angalia ikiwa imani iyo hiyo iliyokaa ndani ya wanawake kama mwanamke Mshunemi, ingali inakaa ndani ya watu leo hii. Mara moja moja, wangeweza kufikia kitu hicho fulani. Si kujiwekelea, sio imani ya kujifanya; bali kitu kilicho halisi, kitu ambacho ni—ambacho ni cha kweli. Hivi hufikirii kwamba tunaweza kufanya hayo usiku wa leo? [Kusanyiko linasema, “Amina”—Mh.]

²⁷⁸ Sasa tunaenda kuombea wagonjwa, tukiweka mikono juu yao, katika Jina la Bwana Yesu, kuwaombea. Sasa labda tunaweza kumalizana na mstari katika yapata, loo, labda dakika ishirini, thelathini. Sasa hatuwezi kusimama kwa ajili ya utambuzi, kwa kweli mnaelewa hilo, maana itazidi. Bali tunaenda kuomba na kuweka mikono juu ya wagonjwa. Je! uko tayari usiku wa leo? Je! unahisi, moyoni mwako, kitu fulani kimekolea, Uwepo?

²⁷⁹ Ni wangapi wamekuwa hapa katika mikutano kote katika juma, hebu tuone mikono yenu. Nadhani kabisa ni nyinyi nyote. Vema. Ni wangapi ambao hawajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano hapo kabla, inueni mikono yenu. Vema, jamani, hao ni nusu. Vema, nadhani wengine hawawezi kuingia ndani. Vema, hebu niwaambie tu. . . Bila shaka, baadhi yao huenda wana kadi ya maombi.

²⁸⁰ Uponyaji wa Kiungu ni kitu ambacho Mungu amefanya tayari. Unaona, ni kitu fulani. Tunaamini, nami ninaamini kwa moyo wangu wote, kwamba Biblia ya Waebrania 13:8, “kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” Yeye ni yule yule. Na mimi ninaamini kwamba Uhai uliokuwa ndani ya Kristo unapaswa kuwa ndani yetu, ikiwa sisi ni Wakristo. Na Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya.” Kasema, katika Yohana Mtakatifu 5:19, “Sitendi lolote mpaka Baba anionyeshe Mimi.” Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁸¹ Sasa hapa, kwa mfano, hapa. Kila mmoja wenu, kadiri nijuavyo, ni wageni kwangu. Vema, ninataka kila mtu kuwa na kicho kabisa kwa kitambo. Na iwapo Yesu Kristo hataonekana miongoni mwetu, katika Nguvu Zake zile zile, basi mimi ni nabii wa uwongo, msinisikilize tena.

282 Ni wangapi hapa hawana kadi ya maombi, hutakuwa kwenye mstari wowote wa maombi, inua mkono wako, popote ulipo. Wewe angalia huku, na uombe kwa moyo wako wote, na uamini. Hii ni ninii ngumu. . . Sikuwa, sikuja nimejiandaa kwa ajili ya hii sasa, lakini ninajua hatuna muda mwingi sana wa kukaa hapa.

283 Sasa ninaenda kuchukua kila roho hapa ndani chini ya udhibiti wangu, katika Jina la Yesu Kristo. Sasa kaeni kwa utulivu. Na iwapo huamini, mbona, afadhali uendelee kuinamisha kichwa chako, unaona. Unaona?

284 Lakini ikiwa wewe ni mwaminio, Biblia ilisema kwamba, “Yeye ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Na Yeye alifanyaje wakati yule mwanamke alipomgusa Yeye? Aligeuka na kujua alikuwa ni nani, na ni nini kilichokuwa shida yake. Alitambua mawazo ya moyo wao. Hivi hamwamini Yeye ni yule yule leo na hata milele? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kama una haja, wewe omba sasa. Na ni nini. . .

“Unazungumzia nini, Ndugu Branham?”

285 Kama mimi ni mtumishi Wake, na ninadai kwamba uhai Wake uko hapa *ndani*, basi kazi zile zile zitajidhihirisha. Sasa, unajua mwanadamu hawezi kufanya mambo hayo. Haiwezekani. Bali Kristo anabaki yeye yule. Na mimi ninawatakeni kuamini hilo.

286 Popote katika jengo, ninawatakeni muwe na imani katika Mungu na mwamini tu, na wewe useme, “Bwana Yesu, mtu huyu hanijui. Na nimekuwa nikisikia kuhusu hili, lakini labda ni hivyo, na huenda ikawa. Sijui. Bali ninajua hanijui. Na ninajua kama angeweza kuniambia. . . Sasa yeye anasema, ‘Uponyaji wako umefanyika tayari.’”

287 Kama Yesu alikuwa amesimama hapa sasa, amevaa suti hii, ambayo Yeye alinipa, Yeye asingeweza kukuponya. Ni wangapi wanajua hilo, enyi wasomi wa Biblia? La, Yeye tayari amefanya hivyo. Unaona? Unaona? Angeweza kuthibitisha kwamba Yeye alikuwa ni Yesu, yeye yule jana, leo, na hata milele; si kwa makovu ya msumari. Uzima Wake! Mtu yeyote angeweza kuwa na makovu ya msumari na kuwa na nywele ndefu, labda, na ndevu. Hata hatujui Yeye alivalia hivyo. Tusingeweza kusema kwamba hiyo ilikuwa sahihi. Unaona? Bali mtu yeyote angeweza kufanya hivyo. Bali Uhai Wake ndio ulio, Uhai Wake ndani yako.

288 Sasa wewe omba, na useme, “Bwana Yesu, jalia nikuguse Wewe,” na uone ikiwa Yeye anabaki yule yule jana, leo, na hata milele. Kama Yeye ataifanya, je! utaamini? Unajua hivyo ndivyo Yeye alifanya. Hiyo ilimthibitisha Yeye kuwa Masihi.

289 Maskini mama huyu aliyeketi hapa, anaendelea kunitazama, na kuweka mikono yake juu ya uso wake, na kadhalika. Una ninii. . . Huna kadi ya maombi, nadhani. Wewe, ninamaanisha maskini mama huyu, huna kadi ya maombi. Hapana. Vema,

je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Ikiwa Bwana Yesu Kristo basi. . . Hatufahamiani kabisa, sisi ni—sisi ni jamii tofauti, mmoja na mwenzake. Lakini kama ninaweza tu kuzungumza na wewe.

²⁹⁰ Aliyeketi mbele yako ni rafiki yangu msiri, Bw. Dauch, kutoka chini huko Ohio, aliyekuwa na kusita kabisa kwa moyo, si muda mrefu uliopita, kwenye umri wa miaka tisini na moja. Madaktari walimkatia tamaa, na kila kitu. Nilitoka nimfikie. Yeye ni ndugu mpendwa, yeye na mke wake mpendwa, anayeketi pale. Wao ni rafiki zangu wasiri. Ndipo nikaondoka ili kumwendea. Na nilikuwa tu ninakuja kutoka kwenye kituo cha petroli, nikijaribu kumfikia, yapata ninii kadhaa, maili mia tatu kutoka kwangu. Nami nilikuwa ninaendesha motokaa kwa kasi nilivyoweza, kuweza kumfikia, maana yeye. . . Mke wake alinipigia simu, kasema, “Bill yuafa.” Kusita kabisa kwa moyo, na mshtuko wa moyo, na umri wa miaka tisini na moja. Ndipo nikaanza kutoka kwenye kituo cha petroli, nikamwona Bill amesimama mbele zangu, akitembea kunijia, mtaani. “Nilikuja na BWANA ASEMA HIVI. Hatakufa.”

²⁹¹ Hapa ameketi papa hapa sasa. Hiyo imekuwa ni miezi iliyopita. Ana imani nyingi. Ameketi karibu na mwanamke huyu. Mwanamke huyu ameketi moja kwa moja nyuma yake. Anaamini. Mwanamke huyo anaamini, pia.

²⁹² Sasa, sikujui. Lakini ikiwa Yesu Kristo. . . Huku, tunaongea sasa kama vile Bwana wetu alivyoongea na yule mwanamke kisimani. Kama Yeye ataniambia kilicho shida yako, kile unachohitaji, au kitu fulani, vema, utajua kama ni Kweli au si kweli, sivyo? Ni kwa ajili ya mwana, na huyo mwana ana ugonjwa wa akili. Ni. . . Kama hiyo ni kweli, inua mikono yako, kama hiyo. Hiyo, hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Vema. Kama utaamini kwa moyo wako wote, na kuchukua hiyo skafu ambayo umepangusa nayo uso wako, uiweke karibu na yeye, na usitie shaka, ugonjwa huo utamwacha. Sasa Mungu yeye yule ambaye angeweza kukuambia. . . Usitie shaka. Hivi huwezi kuona kilichotendeka?

²⁹³ Angalia moja kwa moja—moja kwa moja mwanamke huyu, anayeenda moja kwa moja mahali pake pa kuketi hapa, ma—mama mweusi. Sikujui. Lakini kuna kitu unachotamani. Na mimi nikiwa mgeni, jamii nyingine; kama tu vile Bwana wetu na yule mwanamke kisimani, mmoja Myahudi, na huyo mwingine Msamaria. Iwapo Mungu. . . Je! una kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi. Ninamaanisha maskini mama huyu aliyevalia vazi jekundu lenye milia, papo hapo. Naam. Vema. Si—si—sikujui. Hatufahamiani kabisa. Je! hiyo ni kweli? Na sasa ikiwa Mungu anaweza kunifunulia shida yako, au kitu fulani, na wewe unajua kama ni kweli au si kweli, sivyo? Kusema kweli, huna shida yoyote, ila tu una moyo wenye njaa. Unatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ndipo

utapokea Huyo, hiyo ni kweli, kama utaamini kwa moyo wako wote. Usitie tu shaka. Kuwa na imani katika Mungu. Amina. Naam. Unaamini kwa moyo wako wote? Ninakutaka uamini kwa yote yaliyoko ndani yako.

²⁹⁴ Huyu hapa mama aliyeketi hapa, akinitazama moja kwa moja, moja kwa moja kwenye hayo marefu hapa. Anaugua ugonjwa wa moyo. Ninatumaini hataikosa. Mungu, aniambie ni nani. Yeye ni Bibi Fitzgerald. Je! unaamini kwa moyo wako wote? Unaweza kupata uponyaji wako. Inua mkono wako. Mimi ni mgeni kwako. Je! hiyo ni kweli? Ugonjwa wako wa moyo umekwisha. Je! hilo ndilo jina lako? Hiyo ni kweli. Sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu.

²⁹⁵ Mama huyo moja kwa moja nyuma yako, yeye ana imani nyingi sasa. Anayo kadi ya maombi mkononi mwake, lakini mama huyo anateseka. Na kwa kuwa Hiyo ni Roho Mtakatifu, Nuru hiyo inayoning'inia juu ya mwanamke huyo bado. Yeye anaugua. . . Ana kivimbe katika shingo yake. Na pia ana tumbo lililoshuka. Hiyo ni kweli, sivyo? Iweke tu kadi yako ya maombi sakafuni, huihitaji tena. Mwamini Mungu. Amini.

²⁹⁶ Je! unaamini kwa moyo wako wote? Unaona? Kuwa tu na imani. Usitie shaka.

Hapa yupo mwanamume moja kwa moja hapa nyuma, ana kivimbe.

²⁹⁷ Unaona, pepo huyo, alidhanja angeikosa basi. Yupo mwanaume anayeketi papa hapa, aliye na kivimbe. Kivimbe hicho kiko mgongoni mwake. Simjui mtu huyo. Sijawahi kumwona. Yeye ni mgeni kabisa kwangu mimi. Lakini wakati nilipoona pepo huyo akienda huko nje, kivuli hicho cheusi; na ndipo nikamwona akikimbia huku, akaenda kwa huyu, kwa ajili ya rehema. Wanajaribu kukusanyika kuzunguka hapo. Shetani alifikiria yeye angekosa hiyo, unaona, nilikuwa nimeikosa. Bali Bwana akanionyesha.

²⁹⁸ Mwanaume huyu aliyeketi papa hapa, ana kivimbe mgongoni mwake, na jina lake ni Bw. Carson. Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako, na uponywe katika Jina la Yesu Kristo.

²⁹⁹ Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Iweni na imani. Ikiwa wewe. . .

³⁰⁰ Huyu hapa mwanamke ameketi hapa. Ana ugonjwa wa figo. Ana matatizo. Jina lake ni Bibi Byrd. Hiyo ni kweli. Je! hilo ndilo jina lako, mama? Mimi ni mgeni kwako, je! hiyo ndiyo shida ambayo umekuwa nayo? Kama ndiyo, simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako, katika Jina la Yesu Kristo.

³⁰¹ Nenda kawaulize watu hao. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hivi ham—hivi hamtambui kwamba Uwepo Wake upo hapa?

302 Huyo alikuwa ni mwanangu akiniambia, “Afadhali usiendele.” Unaona, ninao mkutano kesho, na kesho, na kuendelea na kuendelea, unaona.

303 Ninamsai mwanaume au mwanamke yeyote hapa ndani kuamini. Usingeweza kuficha maisha yako kama ilikubidi kufanya hivyo sasa, katika Uwepo wa Mungu. Hilo hasa ndilo Bwana wetu alilotenda. Hilo hasa ndilo aliloahidi katika siku za mwisho. Hilo hasa ndilo lililotendeka kabla ya kuteketezwa kwa Sodoma. Hilo hasa ndilo ishara ya mwisho ambayo ingelijia kanisa. Tupo hapa sasa kwenye wakati wa mwisho. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

304 Ni ipi namba ya kadi yako ya maombi? [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Vema, nitawaambieni kitakachokuwa bora kuliko vyote, hebu tuchukue watu kwa sehemu. Anasema zipo kadi nyingi za maombi. Sasa nyinyi tambueni Mungu yupo hapa.

305 Sasa je! kuna wahudumu wowote? Hii ni sawa, Ndugu Vick? Je! kuna wahudumu wowote hapa, ndugu? Sasa ninaweka mikono juu ya watu hawa, sitaki watu hawa waende, waseme, “Ndugu Branham alifanya hili.” Unaona? Mimi—mimi ni ndugu yenu tu. Mchungaji wenu ana haki sawa tu kuwaombea wagonjwa kama niliyo nayo.

306 Huenda asiwe na karama hii; la, yeye hana, unaona. Kuna mmoja wao tu ulimwenguni, kwa wakati mmoja. Hiyo hasa ndiyo Biblia iliyosema, unaona. Hiyo ni kweli. Na, hiyo, sasa angalia.

307 Bali mchungaji wenu amewekwa na Mungu, kama yeye ni mwaminio, kuwaombea wagonjwa. Na mimi ninawaomba baadhi yenu ndugu wahudumu kuja hapa na kusimama pamoja nami huku tunapoomba; hebu baadhi ya ninii ambao Mungu, wahudumu waliojazwa na Roho wanaoamini katika maombi kwa ajili ya wagonjwa, pamoja na Ndugu Vick, Ndugu Boze. Yuko wapi Daktari Lee Vayle na baadhi yao ambao watakuja hapa, ili kwamba . . . Biblia ilisema, “Ishara hizi. . .”

308 Hebu tusimame papa hapa, ndugu. Vipi kuhusu papa hapa? Njoni moja kwa moja hapa. Naam.

309 “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! mnaamini tuko katika Uwepo wa Kiungu wa Kristo? [“Amina.”] Amina.

310 Niliwatakeni tu mwone. Sababu nilinena jinsi nilivyonena, ilikuwa ni kwa kusudi, unaona, ama kusudi lilitimia vizuri. Mambo makuu yanakaribia kutendeka, ikiwa tu mtaamini.

311 Sasa nitawaambieni kile ninachowatakeni mfanye, ndugu. Ninataka mjigawe nusu upande mmoja, na nusu upande mwingine, mfanye mfano wa uchochoro mdogo unaopitia hapa,

kusudi watu waweze kuja. Ninakuja chini moja kwa moja pamoja nanyi.

³¹² Ninaenda kumwomba mtu ambaye ni mwongoza wimbo, ambaye anaweza kuja hapa, ambaye anaweza kuongoza nyimbo. Ninataka kuteremka huko chini na kuwaombea watu. Mtu fulani anayeweza kusimama hapa na kuwaelekeza watu wanaoenda kuombewa. Asanteni, kwaya, kwa kutupatia. . . Hiyo ni fadhili kubwa kwenu, kutupatia nafasi hiyo kuja namna hiyo. Vema.

³¹³ Hebu wahudumu wapange mstari namna hii tu, sawa. Geukeni, mwangaliane mmoja na mwenzake, mnaona, namna *hii*, na kama mimi na huyu ndugu. Kama mimi na Billy hapa, simameni hivi, mmoja na mwenzake.

³¹⁴ Sasa ni wangapi walio na kadi za maombi upande huu? Hebu tuone mikono yenu. Wapo wengi. Natumai itakuwa vizuri sana kama tungewaacha watokee upande *huu*, na kuja moja kwa moja chini upande huu, namna hii. Sasa kabla ya nyinyi. . . Lakini hebu turuhusu sehemu ya kwanza ya mstari hapa walio na kadi, hebu wapange mstari moja kwa moja hapa juu, na tutaanza kuomba wagonjwa, na kuweka mikono juu yao.

³¹⁵ Sijui ni wangapi hapa, usiku wa leo, ambao—ambao ni wazima na wenye afya, na unataka watu hawa wapate afya? Inua mkono wako. Hakika, mnataka. Sasa, kumbukeni, je! mtaomba pamoja nami? Nyinyi ombeni pamoja nami. Sasa nyinyi ombeni pamoja na wachungaji wenu.

³¹⁶ Sasa kwenu watu wagonjwa ambao mnaenda kupanga mstari na kuombewa hapa. Kumbukeni, mkija kupitia mstari huu, na mimi na hawa wahudumu tuwaguse, kumbukeni, ni tendo tu sawa na ulivyobatizwa. Umekuja, ukiwekewa mikono, na wahudumu waaminio, kwamba, Mungu aliahidi kwamba, “Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Watu hawa walikuja hapa kushuhudia kwamba wanaamini huduma hii. Na wamekuja hapa kama washiriki wake, na sisi pamoja. Sisi sote ni wa nia moja. Tupo mahali pamoja wakati mmoja. Ni wakati sasa kwa ajili ya uponyaji. Bali, ikiwa huamini hilo, usije, maana haitakusaidia hata kidogo. Unaona, huna budi kuliamini. Sasa je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

³¹⁷ Sasa hebu tuinamishe tu vichwa vyetu kwa dakika chache tu. Na tunaenda kuimba pole pole sasa. Kila mtu ukiwa umeinamisha kichwa chako. “Bwana, naamini,” *Amini Tu*, sasa kila mtu pamoja. Hebu tuwe tukiomba sasa, unaona.

³¹⁸ Hebu tuwazie kumwona Yesu akishuka chini kutoka mlimani. Yesu yupi? Yesu yule yule aliye hapa katika umbo la Roho Mtakatifu. Yule yule ambaye anajua kilicho moyoni mwako, kama kweli unaamini au la. Yule yule ambaye anajua yote kukuhusu, anayekwambia usiku baada ya usiku. Ni Yeye. Unajua isingeweza kuwa ni mimi.

319 Na sasa baada ya ninii Yake—Uwepo Wake . . . Sasa, maskini mwanamke Msirofoinike, kumbukeni, baada ya yeye kuingia katika Uwepo wa Yesu, angali alikuwa na shida. Unaenda kuwa na shida. Mnapopitia mstari huu, ninawatakeni, kila mmoja, kuamini kwamba unaenda kupona. Ikiwa huamini, usije. Usi—usichukue tu mahali pa wengine. Kaa hapo mpaka uwe na imani ya kutosha kwamba unaenda kupona, ndipo basi Mungu atakujalia.

320 Sasa wale walio upande wangu wa kulia hapa, pangeni mstari pembeni, wakati sisi wengine tukiimba *Amini Tu*. Wewe uliye na kadi ya maombi, baadhi ya hawa wavulana watakuwa wanasimama Hapo kupokea kadi yako ya maombi wakati unapokuja kwenye mstari, upande huu, upande wa mkono wa kulia. Tokea upande wa mkono wa kulia kama unaweza, maana itawatatanisha, kuanzia upande *huu*. Huwezi kuenda kinyumenyume. Inakubidi kuzunguka *huku*, unaona; inakubidi kuja njia moja, uzunguke. Kama nyinyi ndugu mtanii tu—mtarudi tu nyuma huko na kuwaacha waje kupitia namna hii. Kidogo ni, huenda ikaonekana yenye kutatanisha kidogo, kwa sababu kwamba kuna ku—ku—kundi la watu kushughulikiwa. Bali sasa mwangalieni mwanangu, Billy Paul, waangalieni mabawabu pale; watawaambieni jinsi tu ya kufanya hivyo, hamtachanganyikiwa hata kidogo. Halafu mnaona, upande huu, unapokuja kupitia mstari wa maombi, ndipo utarudi moja kwa moja kwenye kiti chako. Ndipo basi tutachukua upande huu mwingine, na watakuja kutoka upande *ule*, na kupita, mnaona.

321 Sasa tutasimama hapa, vinginevyo tu, mstari, kutoka upande mmoja hadi mwingine, na kuwaombea. Vema.

322 Sasa ninaamini kama nyinyi ndugu mtateremka chini kidogo tu, kusudi ndugu hawa hapa waweze kuingia papa hapa, ili sisi sote tuweze kuwa tukiweka mikono juu ya wagonjwa. Hilo ni sawa tu.

323 Sasa sikilizeni, ndugu, kila mmoja wenu sasa. Kila mmoja wenu ndugu, hivi unatambua kile unachofanya, unaona, unajua mahali ambapo Mungu amekuweka? Sasa hii inaisai imani yako. Kumbuka tu kwamba unaenda kuamini kwamba kila mtu unayemgusa, wewe, hana budi kupona. Inawabidi tu kupona. Mungu alisema hivyo. Ninaenda kuwagusa, pamoja nanyi, nami ninaamini wanarudi kuwa wazima. Hivi hamwamini hilo? [Ndugu hao wanasema, “Amina.”—Mh.] Hebu tuwe tu na maombi miongoni mwetu, huku wengine wenu mkiendelea na kupanga mstari, tunaenda kuiombea hali ya imani yetu wenyewe.

324 Baba wa Mbinguni, wapo watu wengi sana wagonjwa hapa. Na baadhi yao, Bwana, wangali wanaamini kwamba wanapaswa kuwekewa mikono ya wazee. Hilo ni sawa, Baba. Tunajua kwamba Wewe ulifundisha hilo. Ulisema, “Ishara hizi

zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, hao watapata afya.” Uliahidi, na watu wanaamini ahadi yao. Uwepo Wako upo hapa. Hakuna yeyote awezaye kutilia hilo shaka, Bwana. Na hawa hapa wahudumu Wako waliowekwa wakfu wamesimama hapa, waliowekwa wakfu na Roho Mtakatifu, huduma ya kuwaombea wagonjwa.

³²⁵ Sasa, Bwana Mungu, jalia kila mmoja tunayemgusa, usiku wa leo, aponywe. Tunaomba maombi ya imani kwa ajili ya hawa sasa. Tunaenda kuamini, kwamba, tunapoweka mikono yetu juu yao, watapona. Amina. Tuweke tayari, Bwana. Ondolea mbali dhambi yetu na u—uovu wetu. Tusafishe na Damu ya Bwana Yesu Kristo, kwamba tuta . . . Mikono yetu si mitakatifu. Ni kupitia utakatifu Wako pekee tunaruhusiwa kufanya hili. Kwa hiyo jalia hilo, Bwana, ninapojikabidhi mwenyewe, pamoja na hili kundi la ndugu, kwamba sisi tupo hapa kuwasaidia watu hawa wapate kuponywa. Tujalie, Bwana.

³²⁶ Na sasa ninawaombea watu, kila mmoja ajaye kupitia mstari wa maombi. Ee Mungu, wanakuja kana kwamba walikuwa wanakuja kwa ajili ya ubatizo wa maji, wanakuja moja kwa moja kwenye meza ya Bwana, wanakuja chini ya msalaba wa Kalvari. Wanapopitia hapa, naomba watambue kwamba Kristo asiyeonekana Ambaye amesimama miongoni mwa ndugu hawa, aliyesimama hapa sasa kuwapatia thawabu ya imani yao. Na mimi ninakabidhi yote Kwako sasa, Baba, katika Jina la Yesu Kristo.

³²⁷ Sasa ninataka kila mtu mwingine, inamisheni vichwa vyenu. Sikiliza kwa makini sasa maagizo yenu. Usipofanya hivyo, wewe unafanya tu ziara, unaona. Sasa kumbuka, kama Mungu ataniruhusu kujua hali na kadhalika, na wewe uamini hilo, unaona, sasa lichukue tu neno langu, inakubidi kuamini kwamba hili linatosha. Kama halitoshi, huenda likakufanya hali mbaya zaidi. Unaona, tengeneza kila kitu! Kama una dhambi maishani mwako, toka kwenye mstari na ukiri hiyo. Na usije kwenye mstari mpaka uwe umepenya kwa maombi. Na kama unaenda kutumia maisha yako kwa jambo jingine kando na utukufu wa Mungu, usije mstarini. Unaona? Kama uko tayari kujiweka wakfu kwa Kristo, kujisalimisha kikamilifu, na umeshawishika kabisa kwamba huyu ni Yesu Kristo, huyu Roho Mtakatifu mkuu hapa; na kwamba unaenda kupokea uponyaji wako unapopita kwenye mstari huu, haijalishi kama unajisikia tofauti, ama nini, unaenda kung’ang’ania kushikilia moja kwa moja kwenye ahadi za Mungu mpaka ushindi uje, kama yule mwanamke tuliyenena habari zake. Je! mnajisikia hivyo, enyi wasikilizaji? Kama unajisikia hivyo, inua mkono wako, useme, “Ninakubali hilo.” [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Sioni sababu yoyote kwa mtu yeyote kutoka hapa akiwa mgonjwa, usiku wa leo.

328 Sasa ninawatakeni, ambao hamko katika mstari, mwombe. Nadhani Ndugu Joseph anaenda kusimama hapa kuongoza uimbaji, na mimi ninaenda kushuka hapa chini, ili niweze kuomba, pia, na kuweka mikono juu ya watu hawa wanapopita.

329 Sasa tazameni, marafiki, ibada zitakuwa kesho usiku. Hatujui ni nini kitakachofanyika, mtu fulani akiponywa, na kupiga mayowe na kumsifu Mungu, na kadhalika. Huenda tusiruhusiwe rasmi kuondoka kwa kitambo sasa, lakini tafadhali kaeni na mwombe pamoja nasi. Tunawahitaji sasa hivi. Ombeni kwamba adui hataweza kurundika shaka lolote katika nia ya watu hawa. Vipi kama huyo alikuwa ni mama yako amesimama hapo, dada yako, mke wako, mume wako, mtoto wako? Ungetaka mtu fulani aombe kwa uaminifu sana. Kumbuka, ni mama ya mtu fulani, dada ya mtu fulani, kaka, mtoto wa mtu fulani, na tunataka kuwa waaminifu kuhusu hili.

330 Basi wakati tunapoomba, ninawatakeni enyi wanaume, kwa moyo wenu wote, mnapoweka mikono yenu juu ya hawa wagonjwa, amini kwamba Mungu anaenda kumfanya mtu huyo mzima, maana wanaenda kuamini hilo.

331 Na sasa, kati ya sasa na kesho usiku, mbona, kabla sijakuja jukwaani, kesho usiku, kunapaswa kuwa na shuhuda mia tatu au mia nne zikiendelea papa hapa, za, “Nilikuwa ninatumia magongo. Nilikuwa, na sina hayo tena. Nilikuwa mgonjwa, mimi si mgonjwa tena.” Katika saa ishirini na nne zijazo, pepo watakuwa wakiondoka mahali hapa, na kwa sababu baraka zimetangazwa juu ya watu.

332 Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu tunapoomba, kila mmoja wanapopitia kwenye mstari sasa. Ndugu, kuweka tu mikono yenu juu ya wagonjwa. Vema.

333 [Ndugu Branham anateremka chini na wahudumu, na anawaombea wagonjwa. Ndugu Joseph Boze anaongoza kusanyiko katika uimbaji. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

334 Hivi hamjisikii sasa hivi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni wangapi wanaamini kwamba umeponywa? [“Amina.”] Wakipitia kwenye mstari wa maombi hapa, tena na tena na tena, ilitokea papa hapa, kwamba, kabla hawajaondoka jukwaani, ninaamini kwamba kila mmoja wenu atakuwa mzima. Loo, ni—ninaamini hilo. Ninakubali hilo kwa ajili yenu. Imani yangu inaambatana na nyinyi, kwamba watapata afya. Je! mnaamini hilo, ndugu? [“Amina.”] Loo, jamani, Yeye si ni wa ajabu!

335 Hebu tuimbe tu sasa sifa Kwake kabla hatujafumukana. Na halafu hebu tuinue tu mikono yetu, na kuwashikilia juu kabisa. Pia, kumbukeni, tumepitia, karibu na msalaba, na hapo ndipo tulipopata Nuru.

Msalabani, . . . tangulia kuona Nuru,
Nao mzigo wa moyo wangu ukatoweka,
Loo, ilikuwa ni hapo kwa imani nilipokea
kuona kwangu,
Na sasa nina furaha siku nzima!
Msalabani, msalabani ambapo nilitangulia
kuona Nuru,
Na mzigo wa moyo wangu ukatoweka,
Ilikuwa hapo kwa imani nilipokea kuona
kwangu,
Na . . .



KUNGAN'ANIA SWA63-1116E

(Perseverance)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 16 Novemba, 1963, katika Marc Ballroom huko New York, New York, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org